

MWAMUZI AMKASIRISHA VAN DIJK LIVER IKILALA

UKURASA 22

**NONDO** wa ACT ataka tume ya kijaji ichunguze matukio utekaji

UKURASA 2

**MOI** yaomba damu, kila siku yatumia chupa 30 kwa wahitaji

UKURASA 4

**MAKALA MAALUMU** Bibi wa miaka 80, wajane hadi vijana waishi kwa kugonga mawe ya kokoto

UKURASA 11

epaper.ippmedia.com
Nipashe MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

Ijumaa Januari 10, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581917
www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Jahazi la Pakistan lanaswa na mzigo wa 'unga' kufuru

**LINA** uzoefu wa miaka 28; shehena nyingine yanaswa ufukweni...*Ukurasa wa 2*



Raia wa Pakistan wakienda katika chumba cha Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam kusikiliza mahstaka yanayowakabili ya uhujumu uchumi na kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilo 22.52 na Methamphetamine kilo 424.77 jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## Mzee Kimiti ahofia CHADEMA kupasuka

**Na Mussa Mwangoka,**
RUKWA



MWANASIASA mstaafu Paul Kimiti (pichani) amesema anasikitishwa na kinachoendelea ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwa kuwa kinatishia kuleta mpasuko mkubwa ndani ya chama hicho.

Kimiti ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, nyumbani kwake mjini Sumbawanga mkoani hapa.

Alisema kuelekea katika uchaguzi wa ndani wa Chadema kumekuwapo kauli zinazoshiria mvutano mkubwa ambao unaweza kuleta mfarakano na mpasuko mkubwa katika chama hicho, kitu ambacho sio kizuri.

"Unajua wakati huo Seri-


ENDELEA UK. 8

## Biteko avunja safu huduma kwa wateja TANESCO

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA ZAGONGANA 'AIRPORT' UK. 24

KATUNI UK. 6



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (Kulia), akiagana na Balozi wa Korea nchini Tanzania Eunju Ahn baada ya kikao chao jijini Dodoma jana, ambapo walijadiliana mambo mbalimbali ya ushirikiano wa kiuchumi ikiwemo miradi mbalimbali ya maendeleo. **PICHA: WIZARA YA FEDHA**

# Jahazi lanaswa likisafirisha dawa za kulevya

**Na Zanura Mollel**

MAMLAKA ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) imekamata jahazi namba B.F.D 16548 lenye usajili wa Pakistan katika Bahari ya Hindi likisafirisha dawa za kulevya aina ya Methamphetamine.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka hiyo, Aretas Lyimo, alisema hayo jana Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari wakati akiwasilisha taarifa ya hali ya ukamataji na udhibiti wa dawa za kulevya kwa mwaka 2024 huku akibainisha kuwa jahazi hilo limefanya kazi hiyo kwa miaka 28.

Alisema jahazi hilo limekuwa likifanya safari zake kutokea Pakistan kupitia Iran kwa lengo la kupakia dawa hizo kisha kusambaza nchi mbalimbali za Afrika, ikiwamo Tanzania.

Mbali na jahazi hilo, alisema raia wanane wa Pakistan walikamatwa na kufikishwa mahakamani jana.

Kamishna Lyimo alisema dawa za kulevya aina ya Heroin na Methamphetamine husafirishwa kwa njia ya jahazi hilo lenye uwezo wa tani nane kwa wakati mmoja.

"Taratibu za kisheria zinaendelea ili pale mahakama itakapojiridhisha, jahazi hilo litataifishwa na kuwa mali ya serikali," alisema Lyimo.

Alisema mwaka 2024, mamlaka ilikamata kilogramu 2,327,983,66 za dawa ya kulevya kulinganisha na mwaka 2023 wakati kilogramu milioni 1.9 zilikamatwa na kwamba kiasi hicho ni kikubwa kuwahi kukamatwa nchini. Alisema dawa hizo zingepenyezwa na kuingia sokoni zingekuwa na athari kubwa kwa taifa.

Lyimo alisema bangi ni dawa ya kulevya iliyoongoza kukamatwa kwa mwaka 2024 ikifuatiwa na methamphetamine, heroin na dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya fentanyl. Pia alisema mara ya kwanza dawa mpya aina ya 3-4 Methylne-Dioxy-Pryovalerone(DMV), ilikamatwa nchini.

"Operesheni iliyofanyika mwishoni mwa mwaka ilihusisha ukamataji wa jahazi. Tulikamata kilogramu 673.2 za methamphetamine na heroin na kati ya dawa hizo kilogramu 448.3 ziliwahusisha raia wanane wa Pakistan katika Bahari ya Hindi zikiwa zimefichwa ndani ya jahazi na kilogramu 224.9 zilikamatwa katika fukwe za Bahari ya Hindi mkoani Dar es Salaam," alisema Kamishna Lyimo.

Katika kuongeza mapambano dhidi ya dawa za kulevya, Lyimo alisema serikali imenunua boti ya doria inayotarajiwa kuanza kufanya kazi pale taratibu zingine zitakapokamilika ikiwemo uandaaji wa kikosi maalum kwa ajili ya kukabiliana na matukio ya uhalifu katika Ziwa Victoria, ikiwamo usafirishaji wa dawa za kulevya.

Alisema katika mwambao wa bahari na maziwa kuna zaidi ya vipenyo 600, hivyo mamlaka imejitika kushiririkiana na mamlaka zingine za kiusalama katika kukabiliana na uhalifu. Pia alisema wananchi wamekuwa sehemu kubwa ya kutoa taarifa wanapobaini uwapo wa uhalifu katika maeneo hayo.

Kamishna Lyimo alisema, asilimia kubwa ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya wamekamatwa lakini wako waliokimbilia nchi za nje huku wakiendelea na biashara hiyo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

ENTRY FREE
VISIT
INTL TRADE EXHIBITION ON FOOD & PROCESSING
PLASTICS & PACKAGING - PAPER & TISSUE
EXHIBITORS FROM AROUND 17 COUNTRIES
FOODPACK 2025
Products on Display:
Biscuits & Confectionery | Cooking Oil | Cartons for Packaging | Dates Dairy & Milk Products | Premixes for Cakes | Premixes for Bakery Paper Disposable Products | Foam Disposable Food Containers Tissue & Napkins | Disposable Tableware | Plastic Food Containers Plastic Juice Containers | Packaging | Rice | Tomato Ketchup | Salt Silos | Vegetables & Fruits Processing Machinery | Water | Weighing Scale
INTERPLAST PACK
Products on Display:
- Air Compressors
- Boilers
- Glue
- Pneumatic
- Hose Reels
- Packaging
- Seasonal Giveaway's
- Reusable packaging
- Polypropylene (PP) Welding Machinery
- POS Materials
- Publishing
- Food Packaging
- Variable Data Printing
- Digital Printing Solution
- UV Printing Digital Solution
- Extruded Polypropylene
- Sheets
- Plastics Printing Plastics Houseware
PAPER & TISSUE
Products on Display:
- Tissue Converting Machines
- Mat Machines
- Paper Products
- Printing
- Packaging
- POS Materials
- Publishing
- Paper Disposable Products
- Foam Disposable Food Containers
- Food Packaging
- Variable Data Printing
- Digital Printing Solution
- UV Printing Digital Solution
Date & Venue
23-25 January 2025
Diamond Jubilee Hall, Dar-Es-Salaam - Tanzania
Timing
10:00 AM TO 6:00 PM
For more info, Please Call
0758 571652 / 0656 482557
11819102

# Nondo ataka tume ya kijaji kuchunguza utekaji nchini

**Na Restuta James**

MWENYEKITI wa Ngome ya Vijana Taifa ACT-Wazalendo, Abdul Nondo, ametoa mapendekezo matano yatakayosaidia kukomesha matukio ya utekaji nchini, akitaka askari polisi kuvaa sare na kujitambulisha wanapokamata raia.

Vilevile, amemwomba Rais Samia Suluhu Hassan aunde Tume ya Kijaji kuchunguza matukio yote ya mauaji, utekaji na utowekaji raia yaliyotokea mwaka jana ili kubaini watendaji wa uhalifu huo na kuwachukulia hatua za kisheria.

Amesema hayo ukiwa umepita mwezi mmoja tangu alipotekwa na watu wasiojulikana Desemba Mosi mwaka jana saa 10 alfajiri katika Kituo cha Mabasi Magufuli kilichoko Mbezi Luis, Dar es Salaam.

Katika waraka wake aliotoa kwenye mitandao ya kijamii na vyombo vya habari jana, Nondo alisema watanzania wanaweza kutokomeza utekaji na mauji kama wataendelea kuonesha kuchukizwa nayo na kuyapinga.

"Mwaka 2025 uwe mwaka wa kudai uwajibikaji juu ya usalama wa wananchi dhidi ya matukio ya utekaji. Watanzania wote bila kujali itikadi ya vyama vyetu tuungane kwa pamoja kufanya tafakuri, tuhoji na tutake uwajibikaji kwa mamlaka na vyombo husika juu ya usalama wetu dhidi ya matukio ya utekaji na mauaji ambayo yalishika kasi mfululizo mwaka 2024 pasi na majibu ya uchunguzi," alisema.

Kuhusu tume ya kijaji, alisema itatoa majibu ya uhakika kwa kuwa miongoni mwa watuhumiwa wa utekaji na mauaji ya raia ni askari polisi.

"Tume huru ya kijaji kuchunguza itasaidia kujua wahusika na kuwawajibisha na itapunguza wimbi la matukio ya utekaji nchini. Tupaze sauti zetu kutaka Jeshi la Polisi kufuata sheria na taratibu wakati wa ukamataji kwa kuvaa sare, kujitambulisha na kueleza sababu za kukamata mtuhumiwa.

"Hii itasaidia jamii na mkamatwaji kutofautisha ukamataji wa Jeshi la Polisi na watekaji wanaojitambulisha ni Jeshi la Polisi bila kuvaa sare wala kuonesha vitambulisho," alifafanua.

Nondo alisema polisi wasipofuata utaratibu huo, hakutakuwa na tofauti kati ya wahalifu na vyombo vya ulinzi na usalama.

"Ni lazima mstari wa utofauti uchorwe ili kuongeza imani ya wananchi kwa Jeshi la Polisi," alisema.

Nondo alipendekeza pia kuwa ni wakati wa watanzania kupaza sauti ili Jeshi la Polisi libakie kuwa chombo pekee cha ukamataji wahalifu nchini.

Nondo alisema ili kuipa polisi nguvu, Sheria ya Usalama wa Taifa kifungu cha 4(3) kinachoruhusu Ofisa Usalama wa Taifa kukamata mwananchi bila kutoa maelezo ya kosa wala anakompeleka, kinapaswa kufutwa.

Alisema kifungu hicho kimeongeza mwanya wa matukio ya utekaji nchini, akifafanua: "Inawezekana kabisa kifungu cha sheria hii kilikuwa na nia njema ila kwa sasa kinatumika vibaya au kuna kikundi cha watu kinatumia mwanya wa sheria hii kwa maslahi binafsi.

"Ni muda sasa watanzania tuungane kuitaka serikali na Bunge kufuta kifungu hiki ili mamlaka ya ukamataji yabaki chini ya Jeshi la Polisi tu. Hii itafanya Jeshi la Polisi kuwajibika kikamilifu na pia kuondoa mwanya wa watu au kikundi cha watu wanaotumia sheria hii vibaya," alishauri.

Nondo alisema njia nyingine itakayokomesha utekaji na mauaji ya raia ni chombo huru cha kiraia cha kupokea malalamiko ya wananchi dhidi ya matendo ya Jeshi la Polisi, ambacho pia kitachunguza mwenendo wa utendaji wa jeshi hilo.

"Chombo hiki kitasaidia kuwajibisha Jeshi la Polisi, kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, taratibu, taaluma, haki na kulinda utu," alisema Nondo.

Kuhusu kutekwa kwake, alisema waliomteka walimwonya asiseme kilichomkuta wala kuendelea kuandika mitandaoni na kwamba akifanya hivyo watamteka na kumuua.

Alisema tukio hilo lilihatarisha maisha yake kiasi cha kusababisha figo yake moja kufeli kukaribia kushindwa kazi.

"Figo yangu ambayo ilikuwa inakwenda kufeli (Renal Failure) inaimarika na kufanya kazi, majeraha ya mwili, miguu na mikono kuendelea kuimarika sasa ninaendelea na matibabu nikiwa nyumbani na ninaimarika kiafya kwa uwezo wa Mungu," alisema Nondo.

Alisema ameshakiuka masharti aliyopewa na watekaji kwa kuwa hawezi kuacha kuwatetea vijana na kutoa maoni na mawazo kwa ustawi na maslahi ya jamii na Tanzania.

"Ikiwa wataniteka tena na kuniua kwa kuvunja masharti yao kama walivyoahidi, basi na iwe hivyo ili maandiko ya Mungu yatimie ya kwamba kila nafsi itaonja umauti. Utofauti wa mawazo, itikadi au fikra havipaswi kuwa tiketi ya kuteka au kuua mtu yeyote," alisema.

Nondo alisema upande usiopendezwa na maoni au mawazo mbadala, unapaswa kufuata sheria na mifumo ya haki kumshughulikia mtu anayeonekana kutenda uhalifu na si kumteka.

HABARI KITAIFA

## Biteko acharuka utendaji mbovu nakuagiza kuvunjwa kitengo TANESCO

**Na Beatrice Moses**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameagiza kuvunjwa kwa Kitengo cha Huduma kwa Wateja cha Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) baada ya kushindwa kutekeleza maagizo aliyotoa mwaka 2024.

Miongoni mwa maagizo aliyotoa Dk. Biteko alipofanya ziara kwenye kituo Aprili 4, 2024 Dar es Salaam ni kuwaondolea gharama za mawasiliano ya simu wateja kwa kuweka namba ya simu ya bure wanapowasilisha malalamiko kwa mambo yanayowakabili kulingana na huduma zinazotolewa na shirika hilo.

Katika ziara yake aliyoifanya jana kwenye kituo hicho, aliwaeleza uongozi wa TANESCO kuwa amekuwa akiwafuatilia kwa karibu, ikiwamo kupiga simu mwenyewe na amejisikia vibaya wananchi wanapotozwa gharama za simu na mbaya zaidi hawapati huduma waliyoitarajia.

'Mtu anapopiga simu anajua 'seriousness' (umakini) ya Tanesco kwa simu anayopiga. Hapa leo (jana) haipatikani, nikimpigia meneja wa mkoa ndani ya muda mfupi tayari karekebisha. Actually (ukweli) nawaamini mameneja wa mikoa kuliko nyie hapa. Hatuwezi kukubali jambo hili liendelee. Tafuteni uongozi mpya muweke hapa. Ndani ya wiki nataka hapa pasukwe upya. Nataka nione wananchi wanahudumiwa," alisema.

Alisema makadirio ya bajeti ya kufanikisha ufungaji wa simu hiyo ya bure kwa wateja ni Sh. milioni 200 ambayo shirika hilo linamudu, hivyo alitoa wiki moja kufanikisha jambo hilo kuanza.

Dk. Biteko alisema kuwa anatambua malalamiko yameongezeka kuhusu huduma za Tanesco, ambao wamekuwa wakidai kuwa ni kutokana na mifumo kuwakwamisha.

"Hii mifumo nani anayeisimamia kwa nini mifumo ni TANESCO tu. Kwa nini kampuni zingine hazina malalamiko mifumo ni TANESCO tu? Yaani ukipiga simu tu, hata mimi napiga simu, mnaanza kuniambia mmepokea 2,500. Hata mwaka jana mlinimbia hivyo, mliniambia mnataka kuongeza, mnasubiri mitambo mwaka mzima!" alisema.

Aidha, katika maagizo hayo, alitaka ripoti ya taarifa kila wiki ya kituo cha huduma kwa wateja ianze kutolewa ili kufahamu maeneo yenye changamoto ya umeme nchini na kuchukuliwa hatua kwa watendaji wazembe kwenye maeneo husika.

Pia alitaka kila mkoa ulioko chini ya TANESCO, ufanyiwe tathmini kujua umeme umekatika mara ngapi pia kufahamu sababu za kukatika katika maeneo hayo, ili kama kuna uzembe umefanyika serikali ichukue hatua haraka.

***Kwa maoni: +255 677 020 701***
***Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Mbunge wa Jimbo la Tanga, Ummy Mwalimu (kushoto) akizungumza na Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega wakati alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa barabara ya Tanga-Pangani hivi karibuni. **PICHA: OSCAR ASSENGA**

# Kigogo CHADEMA ang'olewa tuhuma kutumia matusi wakati wa kampeni

**Na Waandishi Wetu**

KAMATI ya Utendaji ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Serengeti imemvua uongozi Mwenyekiti wa Chama Mkoa wa Shinyanga, Emmanuel Ntobi kwa madai ya utovu wa nidhamu dhidi ya viongozi wa chama hicho.

Mwenyekiti wa Baraza la Uongozi la CHADEMA Kanda ya Serengeti, Lucas Ngoto amewaambia waandishi wa habari mjini Tarime kuwa uamuzi huo umefikiwa kutokana na kauli na maandiko kadhaa ya Ntobi yasiyokuwa na utu na heshima kwa viongozi wa chama ngazi ya kitaifa.

Alisema katika kikao kilichoketi Shinyanga siku ya Jumatano Januari 8 mwaka huu, wajumbe kwa kauli moja walithibitisha tuhuma nne, ikiwa ni pamoja na kukiuka maadili na kuchafua viongozi wa chama kitaifa kupitia mitandao ya kijamii.

Alisema wajumbe pia walihoji mbinu zake mitandaoni kumuunga mkono mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti Taifa, Freeman Mbowe, wakidai zimekuwa zikichafua taswira ya mgombea mwenzake, Tundu Lissu kwa kutumia lugha za matusi.

"Hii si mara ya kwanza kiongozi huyo kuchukuliwa hatua na chama ngazi ya mkoa na kanda. Mwaka 2023 alisimamishwa uenyekiti kwa mwaka mmoja kutokana na makosa ya kinidhamu," alidai Ngoto.

Alidai Ntobi amekuwa na mfululizo wa maandiko kadhaa, yenye nia ya kumchafua, kumtweza na kumtusi Makamu Mwenyekiti wa Chadema Taifa, Lissu.

Alitaja baadhi ya kauli za Ntobi zilizothibitishwa na wajumbe hao ni pamoja na kumwita Makamu Mwenyekiti Lissu mropokaji na mmbea, na kumtuhumu mara kwa mara kwa mambo ambayo walidai si ya kweli kinyume cha utaratibu na kanuni za chama.

Mratibu wa kampeni wa Lissu na John Heche mkoani Mara, Mwita Isasi alisema wanachama wote wana haki ya kuunga mkono upande wowote pasipo kutumia lugha za matusi na kashfa.

Hata hivyo, Ntobi aliiambia Nipashe jana kuwa mchakato huo haujafuata taratibu za chama, hivyo atakata rufani kupinga uamuzi huo.

"Tuhuma hizo ni matokeo ya joto la kisiasa kutokana na msimamo wangu wa kumuunga mkono moja kwa moja Mwenyekiti wa Chama Taifa, Freeman Mbowe anayetetea kiti chake.

"Sijapelekwa kwenye Kamati ya Maadili, hili ni joto kubwa la kisiasa kufuatia uchaguzi unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni," alidai Ntobi huku akisisitiza kukata rufani kupinga uamuzi huo.

Wakati hali ikiwa hivyo Kanda ya Serengeti, CHADEMA Mkoa wa Singida wametoa tamko la kumuunga mkono Lissu katika uchaguzi wa Mwenyekiti wa Chama Taifa unaotarajiwa kufanyika Januari 21 mwaka huu.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Omari Toto, aliwaambia wanahabari jana baada ya kikao cha viongozi kutoka majimbo yote ya mkoa huo, alisema zipo sababu kadhaa ambazo zimewasukuma kumuunga mkono Lissu, zikiwamo fedha za ruzuku zinazotolewa kwa chama.

Toto alisema CHADEMA kila mwezi imekuwa inalipwa Sh. milioni 107 kama ruzuku ya chama lakini katika hali ya kushangaza fedha hizo zimekuwa zikiishia makao makuu bila kupelekwa mikoani kwa ajili ya maendeleo ya chama.

"Sisi wapigakura ni sawa na kocha, kocha anapoona mchezaji fulani amechoka anamwingiza mwingine ili aweze kupata matokeo mazuri katika timu. Kwahiyo sisi kama kocha, tunasema Lissu ndiye mchezaji wetu atakayekiongoza chama vizuri kwa maendeleo," alisema.

Hata hivyo, muda mfupi baada ya tamko hilo, Mwenyekiti wa CHADEMA Jimbo la Singida Mjini, Swahib Mohamed, alisema anamuunga mkono Mbowe, akidai kuwa kikao kilichoitishwa kimehudhuriwa na watu ambao wengi wao siyo wapigakura wa Mkutano Mkuu.

***Imeandaliwa na Ambrose Wantaigwa (TARIME) na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA)**


Maisha Bila Makato
azam Pesa
Tuma Pesa Bure

ADA ZA WATEJA

piga *150*08#

| KIWANGO (TSH) | KUTUMA PESA KWENDA AZAMPESA (TSH) | | | KUTUMA PESA KWENDA MITANDAO MINGINE (TSH) | | | KUTUMA PESA BENKI (TSH) | | | KUTOA PESA (TSH) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA |
| 0 - 999 | BURE | BURE | BURE | 8.5 | BURE | 8.5 | 51 | BURE | 51 | 150 | 10 | 160 |
| 1,000 - 1,999 | BURE | BURE | BURE | 12.75 | BURE | 12.75 | 85 | BURE | 85 | 242 | 10 | 252 |
| 2,000 - 2,999 | BURE | BURE | BURE | 29.75 | BURE | 29.75 | 170 | BURE | 170 | 349 | 10 | 359 |
| 3,000 - 3,999 | BURE | BURE | BURE | 38.25 | BURE | 38.25 | 170 | BURE | 170 | 486 | 14 | 500 |
| 4,000 - 4,999 | BURE | BURE | BURE | 57.8 | BURE | 57.8 | 340 | BURE | 340 | 567 | 27 | 594 |
| 5,000 - 6,999 | BURE | BURE | BURE | 68.85 | BURE | 68.85 | 340 | BURE | 340 | 734 | 54 | 788 |
| 7,000 - 9,999 | BURE | BURE | BURE | 153 | BURE | 153 | 340 | BURE | 340 | 822 | 56 | 878 |
| 10,000 - 14,999 | BURE | BURE | BURE | 153 | BURE | 153 | 850 | BURE | 850 | 1,123 | 102 | 1,225 |
| 15,000 - 19,999 | BURE | BURE | BURE | 420.75 | BURE | 420.75 | 850 | BURE | 850 | 1,129 | 195 | 1,324 |
| 20,000 - 29,999 | BURE | BURE | BURE | 420.75 | BURE | 420.75 | 850 | BURE | 850 | 1,254 | 306 | 1,560 |
| 30,000 - 39,999 | BURE | BURE | BURE | 459 | BURE | 459 | 850 | BURE | 850 | 1,575 | 351 | 1,926 |
| 40,000 - 49,999 | BURE | BURE | BURE | 520.2 | BURE | 520.2 | 1,700 | BURE | 1,700 | 2,070 | 419 | 2,489 |
| 50,000 - 99,999 | BURE | BURE | BURE | 573.75 | BURE | 573.75 | 2,380 | BURE | 2,380 | 2,430 | 573 | 3,003 |
| 100,000 - 199,999 | BURE | BURE | BURE | 956.25 | BURE | 956.25 | 2,550 | BURE | 2,550 | 3,285 | 707 | 3,992 |
| 200,000 - 299,999 | BURE | BURE | BURE | 1,224 | BURE | 1,224 | 3,400 | BURE | 3,400 | 4,590 | 821 | 5,411 |
| 300,000 - 399,999 | BURE | BURE | BURE | 1,453.5 | BURE | 1,453.5 | 3,400 | BURE | 3,400 | 5,400 | 838 | 6,238 |
| 400,000 - 499,999 | BURE | BURE | BURE | 1,759.5 | BURE | 1,759.5 | 3,825 | BURE | 3,825 | 5,850 | 982 | 6,832 |
| 500,000 - 599,999 | BURE | BURE | BURE | 1,912.5 | BURE | 1,912.5 | 3,825 | BURE | 3,825 | 6,300 | 1,245 | 7,545 |
| 600,000 - 699,999 | BURE | BURE | BURE | 2,448 | BURE | 2,448 | 3,825 | BURE | 3,825 | 6,750 | 1,532 | 8,282 |
| 700,000 - 799,999 | BURE | BURE | BURE | 3,289.5 | BURE | 3,289.5 | 4,250 | BURE | 4,250 | 6,750 | 1,700 | 8,450 |
| 800,000 - 899,999 | BURE | BURE | BURE | 3,289.5 | BURE | 3,289.5 | 4,250 | BURE | 4,250 | 6,750 | 1,750 | 8,500 |
| 900,000 - 1,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 6,750 | 1,776 | 8,526 |
| 1,000,001 - 3,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 6,750 | 1,875 | 8,625 |
| 3,000,001 - 10,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 7,125 | 2,000 | 9,125 |

| TUKIO | ADA |
|---|---|
| Kuangalia salio/Taarifa ndogo | BURE |
| **TAARIFA YA MWEZI** | **ADA** |
| Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |

Hakikisha namba na majina ya mpokeaji kabla ya kutuma pesa.

Hakikisha unatunza namba yako ya siri, usimpe mtu yeyote namba yako ya siri iwe wakala wa Azampesa au mfanyakazi wa Azampesa.

Mteja unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutuma au kutoa hadi Tsh 5,000,000 kwa siku.

MALIPO YA AZAMPESA
Huduma Za Azam, LUKU, Bili Za Maji, Ada Za Shule, Tiketi za Ndege, Mafuta, Manunuzi, Migahawa, Muda Wa Maongezi, Lipa bili, Hisa, Ving'amuzi Vya TV

MALIPO YA SERIKALI

May 2024

GET IT ON Google Play | Download on the App Store

Kwa maelezo zaidi juu ya vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: www.azampesa.co.tz
Huduma kwa wateja, Piga namba 0800 785 555

218319301

HABARI KITAIFA

# Serikali sasa kuifumua reli ya Tazara

Na Halfani Chusi

SERIKALI iko katika mchakato wa kuifumua na kuiboresha upya reli Tanzania na Zambia (Tazara) ili ifanye kazi kwa ufanisi na kutimiza malengo yake.

Jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri wa Uchukuzi, David Kihenzile alisema hayo baada ya kufanya ziara katika makao makuu ya reli hiyo yaliyoko Tazara.

Alisema ziara hiyo ni maelekezo ya Waziri wa Uchukuzi, Makame Mbarawa aliyemtuma kwenda kuangalia ufanisi wake na changamoto zilizopo ili serikali izifanyie kazi kwa haraka.

"Nimesafiri na treni ya Mwakyembe kutoka hapa Tazara mpaka Mwakanga ambapo kuna umbali wa Km 20 kwa lengo la kuangalia utendaji kazi wa treni hiyo," alisema Kihenzile muda mfupi baada ya kushuka katika treni hiyo.

Alisema kuwa katika safari hiyo amebaini watanzania wana imani kubwa na usafiri huo na kwamba katika ripoti ya miaka mitatu iliyopita, abiria walisosafiri wamefika zaidi ya milioni tano inayozidi wale wanaosafiri kwenda Zambia, Kidatu mpaka Makambako.

Kihenzile alisema kuwa kutokana hali hiyo, uwezekzaji wa mabehewa, vichwa vya treni na njia unahitajika lakini tayari serikali ilishayaona hayo na imeanza kuyafanyia kazi.

"Na nimewapa uhakika abiria wetu mnafahamu Rais Samia Suluhu Hassan, miaka miwili iliyopita alifanya ziara Zambia akakutana na Rais wa huko na mwaka jana Septemba marais watatu kutoka China, Tanzania na Zambia walikaa kikao wakakubaliana kwamba lazima reli hii ya tangu mwaka 1975 ifanyiwe maboresho mapya," alisema Kihenzile aliyekuwa ameambatana na baadhi ya maofisa kutoka wizarani.

Alisema reli hiyo ni kongwe na imeharibika sana. Ilikuwa imetengenezwa kubeba mzigo wa tani 5,000,000 lakini ukisoma taarifa ya mwaka jana imefika 447,000 ambayo karibu asilimia tisa ya uwezo wake.

Alisema ukarabarti huo unahitaji muda wa kutosha ili waje na kitu kizuri, akisisitiza lengo lao ni kuwafurahisha wananchi wanaotumia usafiri huo.

Mbali na maeneo ya kufanyiwa ukarabati aliyoyataja Kihenzile, Meneja Mkuu wa Tazara Tanzania, Fuad Abdallah alibainisha maeneo mengine yanayotakiwa kupewa kipaumbele ni uboreshaji madaraja, mahandaki, maeneo ya kubadilishia njia, injini na mabehewa yenye uwezo wa kubeba mzigo mwingi na mzito.

"Sasa tuna changamoto mabehewa ya zamani hayana uwezo wa kubeba kontena nzito, uwezo wa njia ni tani 5,000,000 lakini uwezo wa injini na mabehewa yaliyopo ni tani 500,000," alisema Abdallah.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila (katikati), akiongoza kamati ya maandalizi ya Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Afrika kujadili Nishati (Afrika Heads Of State Energy), utakaofanyika mwezi huu hapa nchini, jijini Dar es Salaam wakati walipokuwa wakikagua miundumbinu mbalimbali kabla ya ujio wa viongozi hao jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kituo mama cha gesi ya magari, bajaji kuanza kazi mwezi ujao

Na Maulid Mmbaga

KITUO Kikuu cha Kujazia Gesi Asilia (CNG Mother Station) kilichoko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kinatarajiwa kuanza kazi rasmi Februari 3 mwaka huu.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, kituo hicho kitakuwa na uwezo wa kujaza magari 1,000 kwa siku, hivyo kusaidia kupunguza msongamano uliopo katika vituo vinne vilivyopo jijini Dar es Salama.

Kumekuwa na changamoto ya msongamano wa vyombo vya usafiri vinavyotumia mfumo wa gesi asilia, hasa bajabi na magari wakati wa kujaza gesi kutokana na uhaba wa vituo husika, jambo lililolazimu serikali kuongeza idadi ya vituo hivyo kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Akizungumza jana mkoani Dar es Salaam wakati akikagua maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho kinachosimamiwa na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Naibu Waziri Mkuu Biteko alisema ujenzi wake umefikia asilimia 80 unaendelea vizuri na mitambo yote inayohitajika tayari imeshawasili nchini.

"Mkandarasi ametuhakikishia kwamba itakapofika Februari 3 mwaka huu kwa mara ya kwanza magari yataanza kwenda kujaza gesi hapa. Lengo letu ni kuondoa foleni ambazo mnaziona zinajitokeza hapa na pale kwa sababu mwitikio wa watanzania kuhamia kwenye mfumo wa gesi ni mkubwa.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo kwamba tujenge vituo vingi zaidi hapa Dar es Salaam ambayo ndiyo mtumiaji mkubwa wa gesi, hiki ni kituo kimojawapo lakini wakati huo huo vinajengwa vingine, saba mkoani hapa kupitia sekta binafsi," alisema Dk. Biteko.

Aliongeza kuwa nia yao ni kwamba ndani ya mwaka huu, waongeze vituo vingine kutoka vitatu vilivyokuwapo mwaka jana hadi kufikia 15.

Alisema kuwa pia kutakuwa na magari yanayotembeza gesi na kujaza katika magari mengine na bajaji katika mikoa ya Morogoro kimoja na viwili Dodoma, akisisitiza kuwa wanataka kuwahamisha wananchi kutoka kwenye matumizi ya nishati chafu kwenda safi.

Alisema wanataka kuongeza kasi na kuhakikisha kuwa vituo hivyo vinajengwa kwa haraka, huku akiwapongeza TPDC kwa kazi nzuri waliyofanya katika kituo hicho mama ambacho wametoa ufadhili kwa asilimia 100.

Alisema Sh. bilioni 18.9 zinatumia kujenga kituo hicho pamoja na vingine viwili vya Kairuki wilayani Kinondoni na Muhimbili jijini Ilala.

Pia alionesha kufurahishwa na hatua ya TPDC kujengea uwezo kampuni binafsi pamoja na vijana wa ndani, akieleza kuwa asilimia 100 ya wafanyakazi katika ujenzi wa vituo hivyo ni wazawa, jambo lililosaidia pia kutengeneza ajira.

# MOI yaomba watanzania waichangie damu

Na Joseph Mwendapole

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) imewaomba watanzania kujitokeza kuichangia damu ili kuokoa maisha ya majeruhi wanaohitaji huduma hiyo.

Ombi hilo lilitolewa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Uuguzi wa MOI, Cresencia Mwibari wakati akijibu hoja na maoni ya wagonjwa na ndugu wa wagonjwa eneo la kusubiria huduma lililoko katika taasisi hiyo.

Cresencia alisema kuwa uhitaji wa damu ni mkubwa. Kwa siku taasisi hiyo hutumia wastani wa chupa 20 hadi 30 kwa ajili ya majeruhi wa ajali mbalimbali zikiwamo za barabarani.

"Ninapenda kutoa rai kwa watanzania wenzangu kuja kuchangia damu katika taasisi ya MOI, hii ni hospitali ambayo inahudumia majeruhi wa ajali mbalimbali, wagonjwa wanakuja wakiwa wamepata majeraha wamemwaga damu, kwahiyo asilimia kubwa wagonjwa huongezwa damu.

"Taaasisi yetu (MOI) hutumia chupa 20 hadi 30 za damu kwa siku, tukipata watu watakaokuja kuchangia damu itasaidia na damu itapatikana kwa wingi na kutuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, tunaomba watu waje kwa wingi," alisema.

Cresencia aliwakumbusha wachangiaji damu salama wa muda mrefu wanaofika katika taasisi hiyo kupatiwa huduma za matibabu kwenda na kadi zao za uchangiaji damu na kuziwasilisha katika idara ya maabara ya MOI kwa ajili ya kufanyia uhakiki na uthibitisho.

Mmoja wa waliowahi kuhudumiwa na taasisi hiyo, Philimon Ndaki aliwapongeza watumishi wa MOI kwa kumpatia huduma za kuridhisha za matibabu, akifafanua kuwa alifanyiwa upasuaji miaka minne iliyopita na sasa anaendelea vizuri na kuhudhuria kliniki kila baada ya miezi sita katika Taasisi hiyo.

"Nilikuja nikiwa na hali mbaya lakini matibabu ya kibingwa niliyopata hapa yaliniwezesha kupata nafuu kubwa sana na sasa niko vizuri sana, watumishi wa MOI ni wakarimu sana," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## Mwaliko Wa Mafunzo ya Matumizi ya Mfumo Mpya wa Usimamizi wa Kodi za Ndani (IDRAS) – Usajili wa Vyombo Vya Moto na Utoaji wa Leseni za Udereva

***Dar es Salaam, 06 Januari, 2025***

Katika jitihada za kuboresha huduma kwa mlipakodi na umma kwa ujumla, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ipo katika mchakato wa kujenga mfumo wa kisasa wa usimamizi wa kodi za ndani uitwao (IDRAS). Mfumo wa kisasa wa kielektroniki utakaoanza kutumika hapa nchini kwa awamu. Awamu ya kwanza itazinduliwa rasmi na kuanza kutumika katika mwezi **Januari 2025,** ikiwa na moduli zinazohusisha:

1) Usajili na usimamizi wa vyombo vya moto (magari, pikipiki, tela, n.k)
2) Utoaji wa Leseni za Udereva

Ikiwa ni maandalizi ya utumiaji wa mfumo huo mpya, TRA imeandaa mafunzo juu ya mfumo huo kwa lengo la kuwajulisha watumiaji juu ya maboresho yaliyofanyika na kuwawezesha kutumia mfumo huu bila changamoto yoyote. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa njia ya masafa **(virtual training)** ili kuwezesha ushiriki wa watu wengi kwa pamoja. Mambo muhimu yatakayofundishwa ni pamoja na:

i). Utangulizi juu ya sifa za mfumo mpya
ii). Mambo muhimu ya kuzingatia ili kuweza kutumia mfumo mpya
iii). Maombi ya leseni ya Udereva (Leseni ya mafunzo ya udereva (Provisional/Learner driving license), Leseni mpya, kuhuisha leseni, pamoja na maombi ya nakala ya leseni)
iv). Usajili wa shule za mafunzo ya udereva
v). Usajili na usimamizi wa vyombo vya moto (usajili mpya, kubadili umiliki, kubadili taarifa, kubadili mmiliki mwenza, kufuta usajili, kurudia usajili, kufunga/kufungua chombo, kusitisha kwa muda matumizi ya chombo cha biashara, Kurekebisha taarifa za chombo baada ya usajili)
vi). Usajili wa wauzaji wa vyombo vya moto (car dealers)
vii). Usajili wa watengenezaji wa ndani wa vyombo vya moto (local manufacturers)

**Ratiba ya mafunzo ni kama ifuatavyo:**

| Tarehe ya Mafunzo | Namna ya mafunzo | Namna ya Kushiriki Mafunzo | Muda wa Kuanza Mafunzo |
|---|---|---|---|
| 9 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (www.tra.go.tz)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii ***(Instagram:****tratanzania,* ***Facebook:****tratanzania,* ***Twitter:****tratanzania)* <br> 2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 10:00 Jioni |
| 10 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (www.tra.go.tz)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii ***(Instagram:****tratanzania,* ***Facebook:****tratanzania,* ***Twitter:****tratanzania)* <br> 2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 10:00 Jioni |
| 11 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (www.tra.go.tz)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii ***(Instagram:****tratanzania,* ***Facebook:****tratanzania,* ***Twitter:****tratanzania)* <br> 2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 4:00 Asubuhi |

Ikumbukwe kuwa pamoja na mafunzo haya, TRA pia itatoa mafunzo zaidi na kwa makundi mahsusi kwa njia mbalimbali ikiwemo semina, vipindi vya redio na televisheni, vipeperushi na kutoa miongozo ya utumiaji (User Guides). Taarifa juu ya mafunzo zitaendelea kutolewa kwa njia mbalimbali ili kuhakikisha kuwa walipakodi na umma kwa ujumla wanapata elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya mfumo wa IDRAS.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

**Tovuti** : **www.tra.go.tz**
**Namba za Simu Bila Malipo** : **0800 750 075 au 0800 780 078**
**WhatsApp** : **0744 23 33 33**
**Barua pepe** : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**
**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadau washiriki kikamilifu kutangaza vivutio vya utalii

**UTALII** ni sekta muhimu katika mchango wa pato la taifa kutokana na Tanzania kujaliwa kuwa na vivutio mbalimbali kama vile mbuga za wanyama, fukwe na mambo ya kale. Sambamba na vivutio hivyo, kuna maeneo mbalimbali ya kihistoria kama vile ya biashara ya utumwa na vita dhidi ya wakoloni ambayo ni chachu katika kukuza sekta hiyo.

Kwa sasa sekta ya utalii pamoja na maliasili, vinachangia asilimia 21.5 ya pato la taifa, hali inayoonyesha kuwa ni mhimili mkubwa katika maendeleo ya nchi kiuchumi. Utalii pekee, kwa mujibu wa takwimu, unachangia asilimia 17.2 wakati asilimia 4.2 inatokana na misitu na nyuki.

Mbali na pato ghafi la taifa, maliasili na utalii zinachangia asilimia 30.9 ya fedha za kigeni, asilimia 25 zikiwa katika utalii na asilimia 5.9 misitu na nyuki.

Kwa takwimu hizo inaonesha kuwa sekta hiyo inachangia pia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo ya uchumi na kupunguza umaskini miongoni mwa wananchi hasa vijana na wanawake kwa kutoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja. Kwa maneno mengine, utalii ni chanzo kikubwa kwa ajira, hivyo kusaidia katika kupunguza umaskini wa hali na wa kipato.

Kutokana na sekta hiyo kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya uchumi, baada ya kuingia madarakani mwaka 2021, Rais Samia Suluhu Hassan alichukua hatua madhubuti katika kuhakikisha inakua na kuongeza pato la taifa na fedha za kigeni. Kwa kufanya hivyo, Rais Samia kwa kushirikiana na Rais wa Zanzibar, alicheza filamu ya The Royal Tour kwa ajili ya kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko pande mbili za Muungano.

Baada ya kuchezwa kwa filamu hiyo, kumekuwa na ongezeko la watalii wanaofika nchini kutembelea vivutio mbalimbali zikiwamo mbuga za wanyama na fukwe mwanana zilizoko katika pwani ya Bahari ya Hindi na visiwa za Unguja na Pemba.

Akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya maliasili na Utalii Mei, 2024, aliyekuwa Waziri wa Wizara hiyo, Angellah Kairuki, alisema idadi ya watalii kutoka mataifa mbalimbali imeongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 1,808,205 mwaka 2003. Aidha, watalii wanaoingia nchini kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) waliongezeka kutoka 780,000 hadi 927,000 kwa ajili ya kutembelea hifadhi mbalimbali za taifa ikiwamo kupanda Mlima Kilimanjaro.


Pia alisema watalii waliotembelea vivutio mbalimbali waliongezeka katika kipindi hicho kutoka 788,933 hadi 1,985,707 sawa na asilimia 152. Ongezeko hilo pia lilichangia kupaa kwa mapato ya fedha za kigeni kutoka Dola za Marekani bilioni 1.3 hadi bilioni 3.4 sawa na asilimia 161.

Kuwapo kwa hali ya utulivu na usalama ni moja sababu za ongezeko la watalii hao na hivi karibuni Bodi ya Utalii Tanzania imetiliana saini mkataba wa kutangaza vivutio vilivyoko nchini na Shirika la Ndege la Uturuki katika miji 350 duniani. Hatua hiyo pia itaongeza wigo wa watali kuingia nchini na kutembelea vivutio na hatimaye kuongeza pato la taifa na maendeleo ya Uchumi kwa ujumla.

Katika kuhakikisha vivutio hivyo vinaendelea kutangazwa, wadau mbalimbali wanapaswa kushiriki kikamilifu kukuza utalii ikiwamo kuibua vivutio na maeneo ya kihistoria ambayo yatasaidia kuwa chachu kwa utalii na maendeleo ya nchi.

Ni wazi kwamba kuna maeneo mbalimbali yakiwamo yenye mbuga za wanyama ambayo hayatafikiwa na watalii wengi, hivyo ni wajibu wa serikali na wadau wakiwamo sekta binafsi kuibua vivutio hivyo ili kuendeleza sekta ya maliasili na utalii nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





Na Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

# Mwaka umeondoka, watu na ofisi tuhesabu mavuno, kisha tuingie darasa hili tuendelee...

**WATU** wanaojitambua, ni wazi hujiwekea malengo na muda maalum wa kuyatimiza, hutumia mwisho wa mwaka kutathmini na mwanzo wa mwaka (mwaka mpya), kuanza utekelezaji, kulingana na mikakati waliojiwekea.

Mipango ipo katika ngazi mbalimbali kuanzia kwenye familia, vikundi mbalimbali vya kijamii, taasisi binafsi na za serikali na taifa kwa ujumla wake.

Huwa na mipango ambayo hutekelezwa kulingana na malengo husika na matokeo yake, hutarajiwa baada ya muda waliojiwekea.

Katika mipango, ipo ambayo utekelezaji wake na matokeo yake huonekana ndani ya muda mfupi, lakini pia ipo mipango ya muda mrefu ambayo utekelezaji wake unaweza kupangwa kutekelezwa kwa awamu awamu.

Mwaka 2025 ni mpya. Mbali na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hiyo ya kuendelea kuishi, ni wazi kwamba kila mmoja wetu anawajibika kutathimini aliyoyafanya mwaka 2024.

Hapo kuna maswali, je yalikuwa na maendeleo katika ngazi gani, kulingana na nafasi yake aliyonayo kuanzia kwenye ngazi ya kifamilia hadi kwenye uongozi wa taasisi, iwe ya binafsi au taasisi.

Kuanzia mtoto mwenye umri ambao anaweza kuelewa maana ya elimu anapaswa kujitathimini kiwango chake cha ufaulu wa mwaka jana, akilinganisha na mwaka uliopita.

Pia, akaweka dhamira yake ya kutimiza malengo kwenye masomo kwa mwaka huu mpya 2025.

Maisha ni mapambano! Kama kuna mipango ya maendeleo uliipanga au yalipangwa na taasisi, kisha haikufanikiwa, kutokana na changamoto za aina mbalimbali, ni jambo jema kujipanga upya, ikiwamo kubadili mbinu badala ya kukata tamaa.

Kukata tamaa, ni kupishana na mafanikio, kwa kushindwa kuongeza bidii kwa kiwango kidogo.

Katika andiko la Mapendekezo ya Mpango wa Watu Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022-2025/2026, pamoja na mambo mengine kadhaa, limeeleza juhudi kadhaa ambazo zimefanywa kutelekeleza mpango huo.

Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa maji mijini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini.

Mengine ni suala la kuendelea na ujenzi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya mijini na vijijini.

Kutokana na utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo, kumekuwapo matokeo chanya katika viashiria vya maendeleo ya watu.

Hapo inakuwamo kuongezeka wastani wa umri wa kuishi kutoka miaka 66.1 mwaka 2019 hadi miaka 68.3 (2023/2024) na makadirio ya kufikia miaka 68.0 kwa mwaka 2025.

Aidha, wastani wa umri wa kuishi kwa kuzingatia jinsia, unakadiriwa kufikia miaka 70.4 kwa wanawake na miaka 65.5 kwa wanaume mwaka 2024. Huu mfano wa mipango ya mafanikio kwa ngazi ya taifa.

Hivyo, haya katika ngazi familia zinapaswa kuangalia ni wapi zilifanikiwa na kama zilikwama, ilikuwaje zikajikuta kwenye hali ya mkwamo.

Pia, hata viongozi wa taasisi binafsi na zile za serikali nao waangalie ni utekelezaji wa mipango kwenye maeneo yao ya kazi.

Daima usione aibu, kubadili marafiki hasa kama umebaini kuwa wana tabia ambazo zimegharimu mafanikio ya mipango yako kukwama, au hawana ushawishi wa kufanya mambo ya maendeleo zaidi wanaendekeza anasa.

Chukua nafasi ya kutafakari sasa, kwamba je mafanikio yako yanachochewa na mambo gani? Kama kuna kikundi au mtu aliyefanikiwa, usisite kuiga, maana wahenga wanasema kizuri huigwa.

Hivyo, siyo mbaya kuiga mbinu za kuhakikisha unafanikisha mipango yako iliyo ya halali.

**- Mwandishi anapatikana kwa anwani: beamoseka@gmail.com; Soma zaidi makala Uk. 12.**

HABARI KITAIFA

# Mlimba yavunja rekodi utoaji mikopo kwa vikundi

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mlimba, mkoani Morogoro imevunja rekodi kwa kutoa Sh. bilioni 2.2 za mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mikopo hiyo imetolewa mapema wiki hii katika viwanja vya ofisi ya halmashauri hiyo na Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya.

Akizungumza wakati wa utoaji wa mikopo hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Jamaly Abdul, alisema Sh. 1,011,701,575 zinatokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ikiwa ni fedha za mwaka 2023/2024 na 2024/2025 na Sh. 1,194,364,886 zinatokana na marejesho.

Alifafanua Sh. 882,426,584.40 zitatolewa kwa vikundi vya wanawake, Sh. 882,426,584.40 zitatolewa kwa vikundi vya vijana na Sh. 441,213,292.20 zitatolewa kwa watu wenye ulemavu.

Jamaly alisema fedha hizo zitatolewa kwa awamu tatu, ya kwanza itatolewa Sh. 746,795,000.00 kwa vikundi 49 kati ya hivyo 26 ni vya wanawake na 19 vya vijana na vinne vya watu wenye ulemavu.

Alisema kwa sasa wanadai Sh. 109,185,500.00 ikiwa ni marejesho kwa vikundi toka kata za Mchombe, Igima, Mofu na Idete na tayari wahusika wote wameanza kusakwa ili kufikishwa katika vyombo vya kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dunstan Kyobya, akizungumza kwenye hafla hiyo amemwagiza Mkurugenzi Mtendaji kuhakikisha vikundi vyote vilivyopo katika kata zote za halmashauri hiyo vipatiwe mikopo.

Alisema haiwezekani tatizo la kikundi kimoja lisababishe wananchi wengine wenye sifa katika kata ambazo zina vikundi vya wadaiwa kukosa mkopo huo, huku akimtaka kuwa mkali katika ukusanyaji wa marejesho.

Pia, Kyobya ameagiza awamu wa pili ya mikopo hiyo ifanyike kabla ya mwisho wa mwezi huu kwa kuwa inaonesha vikundi vingi vinauhitaji wa mikopo hiyo.



Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Doto Biteko (wapili kulia) akipokea maelezo kutoka kwa Meneja Msimamizi wa Mradi wa Kituo Kikuu cha Kujazia Gesi Asilia (CNG Mother Station) jana, kutoka Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDS) Aristides Katto (wapili kushoto) kuhusu maendeleo ya ujenzi wa kituo hicho kilichopo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kinatarajiwa kuanza kazi rasmi Februari 3, mwaka huu. **PICHA: MAULID MMBAGA.**

# Dk. Chana: Teknolojia itumike ulinzi na uhifadhi wa misitu

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, ameuagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kuongeza nguvu ya matumizi ya teknolojia ya kidijitali katika ulinzi na uhifadhi wa misitu kukabiliana na matukio haramu ya uvamizi na ya uchomaji moto kwenye hifadhi za misitu.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi magari yenye thamani ya Shilingi bilioni mbili kwa Wakala huo, Dk. Chana, alisema kuna umuhimu wa kuja na mbinu mpya za ulinzi ambazo zitasaidia kupambana na matishio kwenye hifadhi hizo za misitu ikiwamo zinazotumiwa na wavamizi haramu.

"Tuna maeneo makubwa ambayo yanahitaji kuhifadhiwa, lakini wakati mwingine tunapungukiwa na rasilimali, hivyo kuna haja ya kuendelea kubuni mikakati mipya ikiwamo matumizi ya teknolojia kudhibiti uharibifu kwenye misitu na kuondokana na changamoto nyinginezo," alisema Dk. Chana.

Dk. Chana aliitaka TFS, kuongeza wigo wa matumizi ya ndege zisizo na rubani (Drone) pamoja na satelaiti kupambana na uharifu kwenye hifadhi ambazo zitatumika kufuatilia na kufanya doria kwenye hifadhi za misitu kwa ufanisi zaidi.

Pia, aliitaka kushirikiana na uongozi wa serikali za mitaa, kuelimisha wananchi wanaozunguka hifadhi hizo, kushirikiana katika suala la ulinzi kwenye hifadhi hizo pamoja na namna ya kuachana na matukio ya uchomaji moto.

"Matukio ya moto kwenye misitu, ndio tishio kubwa katika uhifadhi wa msitu nchini, ni vema kuendelea kutoa elimu kwa wananchi, waache kusafisha mashamba kwa kutumia moto kwa sababu wanapofanya hivyo, unasambaa mpaka kwenye hifadhi," alisema Dk. Chana.

Kadhalika, Dk. Chana aliitaka TFS, kuanzisha kituo cha mawasiliano ambacho kitasaidia kurahisisha namna ya kuripoti matukio ya uhalifu katika hifadhi za misitu nchini.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Kamishna wa Uhifadhi wa TFS, Prof. Dosantos Silayo, alisema jumla ya Sh. bilioni 11.6 zilitengwa kwa ajili ya kununua magari ya kusaidia shughuli za uhifadhi.

Pia, Prof. Silayo alisema wakala huo umefanikiwa kutatua migogoro 423 kati ya 438 inayohusiana na misitu ambayo iliibuliwa katika ripoti tatu za wizara kwa mwaka mzima.

Alisema wageni 100,075 walitembelea hifadhi mbalimbali za misitu nchini ikiwa ni sehemu ya utalii.

KABWELA Na Fadhili Mohammed



# Kimiti apata hofu Chadema kupasuka

**Na Mussa Mwangoka,**
RUKWA

MWANASIASA mstaafu Paul Kimiti amesema anasikitishwa na kinachoendelea ndani ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwa kuwa kinatishia kuleta mpasuko mkubwa ndani ya chama hicho.

Kimiti ambaye ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alisema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe, nyumbani kwake mjini Sumbawanga mkoani hapa.

Alisema kuelekea katika uchaguzi wa ndani wa Chadema kumekuwapo kauli zinazoshiria mvutano mkubwa ambao unaweza kuleta mfarakano na mpasuko mkubwa katika chama hicho, kitu ambacho sio kizuri.

"Unajua wakati huo Serikali na Chama cha Mapinduzi kilipokubali tuwe na vyama vya upinzani, walikuwa na nia nzuri sana vyama vitakavyosaidia kuikosoa serikali au sera zinazoonekana hazisaidii kujenga na kuendeleza umoja na maendeleo ya nchi.

Lakini vyama vyenyewe vikianza kusigana, binafsi sipendi kwa sababu havitujengei ile hali ambayo tunaitegemea kuwa na vyama imara ambavyo vingesaidia kuikosoa CCM.

Alisema yanatokea Chadema ya kuchafuana hadharani ni dhahiri kutatokea mpasuko mkubwa ambao utasababisha baadhi ya wanachama wao kukihama chama hicho na kurudi kule kule ambako vyama vitakuwa havina nguvu ya kuikosoa serikali.

**"Unajua wakati huo Serikali na Chama cha Mapinduzi kilipokubali tuwe na vyama vya upinzani, walikuwa na nia nzuri sana vyama vitakavyosaidia kuikosoa serikali au sera zinazoonekana hazisaidii...**

Alitaka viongozi wa vyama hivyo na wanachama wao kuhakikisha wanafanya uchaguzi wa amani na utulivu, hali ambayo itaepusha uvunjifu wa amani ambao sio kwao pekee bali kwa nchi nzima.

Pia, alitamani nchi kutokuwa na utitiri wa vyama vya siasa badala yake viwapo vichache vyenye nguvu tofauti na sasa kuna vyama vya siasa zaidi ya 17 huku vingine vikiwa havina nguvu ya kisiasa.

Katika hatua nyingine, Kimiti alikemea vitendo vya rushwa ndani ya vyama vya siasa katika kipindi hiki cha kuelekea chaguzi za vyama vya hivyo.

Alisema Baba wa Taifa alikemea rushwa, lakini katika miaka ya karibuni vitendo hivyo vimetamalaki na baadhi ya wagombea wa nafasi mbalimbali wameanza kutoa rushwa ili kupata nafasi kitu ambacho sio sahihi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***



Taka zikiwa zimerundikwa pembeni mwa barabara ya Morogoro eneo la Manzese Argentina kusubiri wazoaji jana. Kumekuwa na uchelewaji wa kuondoa taka na kuharibu mandhari. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TBS yaonya watengeneza maudhui potoshi ya chakula mtandaoni

**Na Jenifer Gilla**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS), limeonya baadhi ya watengeneza maudhui mitandaoni wanaosambaza picha mjongeo (video) potofu za bidhaa za chakula, kuwa sheria kali zitachukuliwa dhidi yao.

Onyo hilo limekuja siku chache tangu kusambazwa kwa picha mjongeo kwenye mitandao ya kijamii ikionyesha mwanamke akisafisha miguu yake ndani ya beseni lenye maembe kisha juisi yake kuiweka kwenye chupa kwa ajili ya kuuzia wateja.

Video hiyo ilileta taharuki kwa jamii na kuzitaka mamlaka kuwachukulia hatua za kisheria watu hao kwa upotoshaji unaoweza kuharibu soko la kinywaji hicho au kuweka afya za walaji katika hatari kama baadhi ya watu wakiamua kuiga tabia hiyo.

Taarifa iliyotolewa na Kaimu Meneja wa Masoko wa Shirika hilo, Debora Haule kupitia mitandao ya kijamii juzi, ilisema limebaini uwapo wa mwenendo wa baadhi ya watengeneza maudhui kusambaza picha mjongeo katika mitandao ya kijamii zinazoonesha maudhui potofu yahusuyo bidhaa za chakula.

Alisema ni kinyume na Sheria za Viwango Sura ya 130.

Aidha, kwa mujibu wa sheria hiyo, hairuhusiwi mtu yeyote kutengeneza, kuandaa, kusambaza, kuuza na kutangaza bidhaa ambazo zinaweza kuathiri afya ya mtumiaji pamoja na maudhui ambayo yanapotosha watumiaji.

"Aidha, hairuhusiwi kutangaza au kuuza bidhaa za chakula katika maeneo ambayo hayajasajiliwa na TBS," alisema.

Alisema shirika hilo litashirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha kuwa yeyote anayetengeneza maudhui ya vyakula kwa nia ya kupotosha jamii anachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria.

Aidha, siku za hivi karibuni kumeibuka tabia ya watengeneza maudhui kusambaza video zinazoonyesha maudhui yasiyokuwa maadili kwa malengo ya kuongeza wafuatiliaji wa kurasa zao.

Januari 7, mwaka huu Jeshi la Polisi mkoani Mwanza lilimshikilia John Isaya (21), dereva bajaji na mkazi wa Mtaa wa Bukala, wilayani Sengerema kwa tuhuma za kutengeneza na kusambaza picha mjongeo katika mtandao wa kijamii (Tik Tok) akitangaza kuwa anauza mtoto wake aliyekuwa amembeba kwa mbeleko kwa Sh. million 1.6.

Matukio hayo ya aina hiyo yalimwimbua Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima na Januari 6, mwaka huu alionya kuwa wizara itawawajibisha wote watakaobainika kuandaa maudhui yasiyozingatia maadili, weledi na miongozo.

Alisema kumeibuka wimbi kubwa la waandaa maudhui hayo mitandaoni, ambalo linafanya kazi zake bila weledi wa aina yoyote na kwamba jambo hilo lina athari kwa jamii.

Alisisitiza kuwa kundi hilo ni muhimu katika jamii ambalo kama wakizingatia weledi, miongozo ya kisera na sheria ya kurusha maudhui mitandaoni kazi zao zitaleta mchango chanya kwenye maendeleo na ustawi wa jamii kwa sekta zote.

# Mil. 75.7/- Mfuko wa Jimbo zanunua vifaa vya ujenzi Shule Musoma Vijijini

**Na Sabato Kasika**

FEDHA za Mfuko wa Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara, Sh. milioni 75.7 zimetumika kununua vifaa vya ujenzi wa shule mbalimbali jimboni humo ikiwa ni sehemu ya kuboresha elimu.

Mwenyekiti wa mfuko huo, ambaye pia ni Mbunge wa Musoma Vijijini, Profesa Sospeter Muhongo alisema hayo alipokuwa akizungumza na gazeti hili jana kuhusu mkakati wa kuinua elimu jimboni mwake.

Alisema wiki iliyopita, Kamati ya Mfuko wa Jimbo ilitembelea ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Musoma zilizopo Kijiji cha Suguti ili kuainisha vifaa vya ujenzi vitakavyonunuliwa na fedha za Mfuko wa Jimbo kwa ajili ya shule mbalimbali.

"Fedha za Mfuko wa Jimbo ni Sh. milioni 75.7, vifaa vya ujenzi vitakavyonunuliwa ni saruji mifuko 1,970, mabati ya rangi 322 na nondo 430 za milimita nane," Prof. Muhongo alisema.

Alizitaja baadhi ya sekondari zilizogawiwa vifaa vya ujenzi kuwa ni Muhoji, Nyasaungu, Rukuba na zinazokamilisha ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi.

"Sekondari zilizokamilisha masomo hayo ni Mtiro, Makojo, Nyambono, Bwai, Mkirira, Etaro na zinazoanza ujenzi wa maabara za masomo hayo ambazo ni Bukwaya na Nyanja," alisema.

Alizitaja nyingine zilizofaidika ni Chitare, Mwigombe, Mmahare, Musanja, Kataryo na Nyabakangara ambazo wananchi wako kwenye harakati wa ujenzi.

"Musoma Vijijini tuna vijiji 68 na sekondari 26 za serikali, huku mbili zikiwa za binafsi, mkakati wa kujenga sekondari kila kijiji, hivyo tunafanya kila njia kufanikisha hilo," alisema.

Ofisa Elimu Sekondari wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma Majidu Karugendo alisema mkakati huo wa kuwekeza kwenye elimu ndio unaopigiwa debe na serikali kila siku.

"Kipaumbele chetu katika maendeleo ni elimu, ndio maana tunaendelea na mkakati wa ujenzi wa sekondari kwa nguvu za wananchi kwa kushirikiana na serikali. Tumshukuru Mbunge Profesa Muhongo kwa kuunga mkono juhudi hizo," alisema Karugendo.

Alifafanua kuwa huenda mwaka huu baadhi ya sekondari zikafunguliwa ili kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza na nyingine kupandisha na kuwa na kidato cha tano na sita kwa mchepuo wa masomo ya sayansi.

Kuna sekondari mbalimbali za vijiji zinaendelea kujengwa zikiwamo za Rukuba Island, Nyasaungu, Muhoji, Butata, Nyamrandirira Technical, David Massamba Memorial, lakini pia kuna sita za vijiji vya Chitare, Kataryo, Kiriba, Mmahare, Musanja na Nyambono ambavyo vimepata vibali vya kuanza kujenga sekondari," alisema.



# Kigogo NLD: Udereva isiwe ajira kwa vijana

**Na Oscar Assenga,** TANGA

WAKATI jinamizi la ajali za barabarani likiendelea kutikisa nchi, Katibu Mkuu wa Chama cha NLD Taifa, Doyo Hassan Doyo, ameshauri udereva isiwe ajira ya vijana bali watu wazima kuanzia miaka 40 na kuendelea.

Jana, Doyo, alisema anatamani vyombo vinavyohusika hasa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini (LATRA), Jeshi la Polisi na Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) kutafakari upya kuhusu umri sahihi wa madereva wa mabasi ya abiria.

Alisema anatamani mabadiliko hayo tofauti na ilivyo sasa, madereva wengi chini ya miaka 25, hawawezi kumudu changamoto za barabarani kutokana na umri na kutokuwa na uzoefu.

**"Niiombe serikali na vyombo vyake, na hata wizara husika iwajibike kuhakikisha madereva wanaoendesha magari ya abiria,**

"Mfululizo wa matukio ya ajali katika kipindi cha mwisho wa mwaka umehusishwa na wingi wa vyombo vya usafiri barabarani, baadhi ya madereva wa magari binafsi kukosa uzoefu na barabara nyembamba.

"Niiombe serikali na vyombo vyake, na hata wizara husika iwajibike kuhakikisha madereva wanaoendesha magari ya abiria, wawe na umri wa utu uzima ili kuepusha ajali ambazo zimekuwa zikitokea na kupoteza maisha ya Watanzania na kuwaachia wengine ulemavu," alishauri Doyo.

Kanzidata ya Jeshi la Polisi, inaonesha ajali za barabarani zilizotokea nchini kipindi cha mwezi Januari hadi Desemba mwaka jana zilikuwa 1,735.

Kwa mujibu wa jeshi hilo, ajali 1,198 kati ya hizo zilisababisha vifo.

Takwimu za jeshi hilo zinaonesha kuwa mwaka juzi, matukio ya ajali za barabarani yalikuwa 1,733 kuanzia Januari hadi Desemba, na kusababisha vifo vya watu 1,118.

Katika salamu za mwaka mpya wa 2025, Rais Samia Suluhu Hassan, alimuagiza Waziri wa Mambo ya Ndani, Innocent Bashungwa na jeshi hilo kuongeza mikakati ya kuzuia ajali hizo za barabarani.

## Waziri akerwa daraja Mto Pangani kusuasua

**Na Mwandishi Wetu,** PANGANI

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega amesema Serikali haifurahishwi na kusuasua ujenzi wa mradi wa ujenzi wa daraja kubwa la Mto Pangani lenye urefu wa mita 550.

Daraja hilo linajengwa kwa miezi 36 kwa gharama ya Sh. bilioni 82.19, ikijumuishwa pamoja kipande cha barabara yenye urefu wa kilomita 25 kwa kiwango cha lami kutoka Bweni hadi Tungamaa.

Waziri Ulega alieleza hayo katika kikao chake cha majumuisho, mkoani Tanga baada ya kutembelea na kukagua mradi huo juzi.

"Kwa mwendo huu sifurahishwi, mkandarasi ni lazima ufanye kazi usiku na mchana ujenzi ukamilike mapema na lianze kutumika. Kwa sababu adhma ya serikali kupitia mradi huu ni kukuza uchumi wa Wilaya ya Pangani na Mkoa wa Tanga.

Hili daraja likikamilika kwa wakati litawezesha wananchi kufanya shughuli zao kirahisi badala ya kutegemea matumizi ya kivuko cha MV Pangani."

Alisisitiza: "Mkandarasi na wasimamizi Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) hakikisheni mnaongeza kasi kwa maana muda wa kufanya kazi uwe usiku na mchana tunataka daraja likamilike mapema watu wa Pangani wanataka wapite hapa waachane na kivuko, hivyo wasilale usingizi."

Waziri huyo, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 4.7 ili Mkandarasi wa Kampuni ya Chiko aendelee na ujenzi wa barabara ya Tanga/Pangani kwenda kuunganisha Banagomo/Makurunge kupitia Sadani.

Baadhi ya wakazi wa Pangani, akiwemo, Mwanaisha Athuman, wa Bweni, alisema daraja hilo lina umuhimu kwa kuifungua wilaya hiyo kiuchumi na kuwaondolea adha wakati kivuko kimemaliza muda wake wa kutoa huduma.

"Daraja lilikuwa ni kilio kikubwa sana kwetu hapa Pangani. Kauli ya Waziri, tunaamini itaharakisha na kutatuondolea adha tuliokuwa tunaipata. Tunaishukuru serikali kwa kutekeleza mradi huu ambao ni muhimu kwa maendeleo yetu wana Pangani," alisema.

Bakari Mwinchande, Mkazi wa Pangani Mjini, alisema wanamshukuru Waziri Ulega kwa kauli ya kuchagiza kasi ya ujenzi ufanyike kwa wakati na ubora ili watumie daraja hilo.




.Wakazi wa mtaa wa Msuguru mwisho wa lami wilayani Muheza Tanga, juzi wakiwa wamepanga foleni ya ndoo na madumu ya kubebea maji kutokana na uhaba wa maji eneo hilo, uhitaji umeongezeka kutokana na wingi wa watu. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## LATRA, Polisi wapiga kambi eneo 'uchovu wa madereva'

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) na Jeshi la Polisi mkoani hapa wamejipanga kufanya doria na ukaguzi wa magari katika barabara kuu ya Segera-Manga mpaka Mombo ili kudhibiti uchovu wa madereva na kuchangia ajali.


Hayo yalisemwa jana na Ofisa Mfawidhi wa LATRA Mkoa wa Tanga, Shedrack Malale katika mahojiano na gazeti hili kuhusu walivyojipanga kudhibiti madereva wanaovunja sheria za usalama barabarani, kusababisha ajali, kupoteza maisha ya watu na mali.

Malale, alisema licha ya kuangalia na kudhibiti eneo hilo alilolitia la uchovu wa madereva, wanafuatilia mwendo wa madereva hasa kwa madereva magari aina ya Coaster maarufu Special Hire kwa kutumia vifaa maalum.

"Hayo tunayafanya kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi hasa katika kipindi ambacho abiria wanaporudi baada ya kumalizika Sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya, tumejipanga kufanya ukaguzi katika maeneo hayo kuhakikisha abiria safari zao ziwe salama zaidi, "alisema.

Malale, aliwataka madereva kutii na kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali.

Tanga ni miongoni mwa mikoa minne iliyopo ukanda wa Kaskazini. Mingine ni Kilimanjaro, Arusha na Manyara.





# M'kiti apasua jipu mapato ya serikali

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Kaliua mkoani Tabora, Raphael Lufungija amesema baadhi ya watendaji wanapoteza mapato ya Serikali na kukwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kukaa na fedha mfukoni badala ya kupeleka benki.

Lufungija ambaye pia ni Diwani wa Kata ya Ilege, Tarafa ya Ulyankulu alibainisha hayo juzi wakati akizungumza na Nipashe na kuwataka watumishi hao kufuata taratibu za ukusanyaji mapato ya serikali na kupeleka kuhifadhi benki.

"Hili halikubaliki, yeyote atakayebainika kufanya upuuzi huu achukuliwe hatua. Watumishi wanatakiwa kutimiza majukumu yao ipasavyo kuhakikisha mapato yote yanayokusanywa kutoka vyanzo mbalimbali yanafikishwa benki," alisema Lufungija.

Hata hivyo, alisema halmashauri hiyo ni miongoni mwa halmashauri nchini zilizopata mafanikio makubwa kutokana na utendaji mzuri wa kazi wa wataalamu wake na timu nzima ya mapato. Alisema pamoja na mafanikio hayo, halmashauri hiyo imeathiriwa na utendaji wa mazoea wa baadhi ya watumishi wake.

Alisisitiza kuwa kama kila mmoja atasimama kwenye kazi yake na kufanya kile kinachotakiwa, halmashauri hiyo itaendelea kupiga hatua kubwa zaidi kwa maendeleo ikiwemo kukusanya zaidi ya Sh.bilioni 10 ya mapato kwa mwaka. Alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Jerry Mwaga kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa kwenye vyanzo vya mapato zinatolewa taarifa na kuhifadhiwa benki mara moja ili kudhibiti upotevu na wizi.

**Alimuagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Jerry Mwaga kuhakikisha fedha zote zinazokusanywa kwenye vyanzo vya mapato zinatolewa taarifa na kuhifadhiwa benki mara moja ili kudhibiti upotevu na wizi.**

Alisema fedha za mapato ya ndani ndizo zinazotumika kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alionya kuwa uzembe katika ukusanyaji wa mapato hayo ni chanzo kwa kukwama kwa utekelezaji wa miradi hiyo katika jamii na kuzua malalamiko kwa wananchi.

Kwa upande wake, Mwaga aliahidi kufanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na mwenyekiti huyo huku akisisitiza wameanza kuchukua hatua dhidi ya wanaokwamisha halmashauri hiyo kupata mapato.

Alisema watendaji na timu nzima ya mapato wanapaswa kushirikiana ili kuvuka malengo yanayowekwa na halmashauri hiyo mwaka.



Wawakilishi wa Taasisi ya Nyansaho Foundation ya wilayani Serengeti mkoani Mara, wakimkabidhi mabati Kassim Matiko (wa nne kushoto) ambaye ni miongoni mwa wakazi wa Kijiji cha Merenga Kata ya Nyansurura ambao nyumba zao ziliezuliwa na upepo uliombatana na mvua hivi karibuni. Kaya tatu zilipata msaada wa mabati, chakula na fedha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Vijiji Bunda kuunganishiwa maji ya Ziwa Victoria

**Na Vitus Audax**

ZAIDI ya wakazi 23,000 wa kata zilizopo pembezoni mwa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda mkoani Mara wako mbioni kupata majisafi na salama baada ya Serikali kuanza kutelekeza Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria mwanzoni mwa mwezi ujao.

Mpango huo ulitangazwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Bunda (BUWSSA), Esther Gilyoma wakati akizungumza kwenye mkutano wa mbunge kusikiliza na kutatua kero za wananchi uliofanyika Kata ya Nyamuswa.

Eshter, alisema serikali kupitia Wizara ya Maji inaendelea kutekeleza miradi ya usambazaji maji kwa wananchi kutoka chanzo cha maji cha ziwa hilo na kufikisha katika makazi yao. "Utekelezaji wa mradi huo, unatarajia kuanza Februari 1, 2025 na kukamilika Januari 30, 2026 kwa gharama ya Sh. bilioni 8.3 fedha kutoka Serikali kuu," alisema.

Alivitaja vijiji vya kata hizo za Nyamuswa na Ketare vitakavyonufaika na mradi huo unatekelezwa na wakandarasi MOLI OIL MILLS na GAT ENGINEERING CO. LIMITED kuwa ni Bukama, Makongoro A, Makongoro B, Nyamuswa na Tiring'ati.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Stafa Nashoni, aliahidi kutoa ushirikiano kwa BUWSSA kufanikisha utekelezaji wa mradi huo na kufikisha maji katika vijiji hivyo kwa wakati.

# Waomba elimu huduma ya 'ambullance'

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga wameomba kupatiwa elimu ya jinsi ya kupata huduma ya gari la wagonjwa ili kuokoa maisha ya wagonjwa na wajawazito maeneo ya vijijini.

Walitoa ombi hilo kwa nyakati tofauti baada ya Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani kukabidhi gari la wagonjwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Ushetu kwa niaba ya Wizara ya Afya.

Mkazi wa Kata ya Nyamilango, Kulwa Samwel, alisema hawana uelewa juu ya upatikanaji wa gari hilo ili kuwawaisha wagonjwa hospitalini kupata huduma ya dharura.

Samwel, alisema baadhi ya wajawazito wanakuwa shambani hadi wanapopata uchungu na hawafahamu jinsi ya kupata msaada wa gari hilo.

"Tunaomba Ofisi ya Maganga mkuu itoe maelekezo ya namna ya upatikanaji wa ambullance ili kuondoa malalamiko ya wananchi hasa kwa wajawazito, watoto pamoja na wazee," alisema Samwel.

Matrida William, alisema gari hilo litakuwa msaada kwa wajawazito kutojifungulia nyumbani nyakati za usiku huku akitaka jamii elimishwe upatikanaji wa huduma hiyo.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Ushetu, Dk. Athman Matindo akitoa taarifa ya hali ya utoaji wa huduma ya usafirishaji wa wagonjwa, alisema zimeimarika kwa wananchi kwa wakati wote katika zahanati na vituo vya afya vilivyopo.

Dk. Matindo, alisema hadi sasa wana magari matatu ya wagonjwa, mawili ya wasimamizi shirikishi mawili na pikipiki 22 katika vituo vya kutolea huduma.

Vilevile, alisema wana gari la kusafirisha wagonjwa nje ya Ushetu kupata huduma zaidi za rufani.

Matindo, alisema mara kadhaa wajawazito wakihudhuria kwenye zahanati na vituo vya afya kujua maendeleo, wanapopata uchungu wa kujifungua wanatoa taarifa na kufuatwa na magari na kuwahishwa kupata huduma.

Mbunge Cherehani, alisema awali hospitali ya wilaya ililazimika kutumia magari ya wagonjwa ya vituo vya afya jirani kusafirisha wagonjwa kwenda Hospitali ya Rufani Mkoa na Bungando jijini Mwanza na sasa adha hiyo haitakuwepo baada ya kupatikana kwa gari hilo.

Alisema hospitali hiyo inahudumia wagonjwa kutoka Wilaya Kaliua, Urambo na Sungwa mkoani Tabora na kumtaka Mganga huyo kuendelea kuwabana watumishi wake kutoa lugha nzuri kwa wangojwa kutokana na baadhi yao kuwa na za kuhudhi na dharau.




Kamwe tusikubali mazingaombwe kwenye uchaguzi



## Akikaribia miaka minne; Samia na staili ya kusuka uchumi kwa nguzo za kiafya, siasa

Ukurasa 12


# BUFE

IJUMAA JANUARI 10, 2025

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA


### KUWA UYAONE MAISHA!

# Bibi miaka 80, wajane, hadi vijana waishi kwa kugonga mawe kokoto

## •Wategemezi kibao, wengi wana ulemavu, kipato...

**Na Pilly Kigome**

KAZI inatajwa kuwa jibu kuu la hatima au kipato cha watu. Hapo ndipo katika dodoso wanapatikana kinamama wanaojishughulisha na ugongaji mawe makubwa.

Ujira wao ni shilingi 250 kwa ndoo, eneo la Kunduchi Mtongani, mkoani Dar es Salaaam wanakiri ni 'kazi ngumu', kukiwapo kundi la wenye umri mkubwa, shida na majukumu kifamilia, zimewaelemea.



Mariamu Shija (80), bibi anayetegemea ujira wake kwa kugonga mawe ya kokoto, mwenye miaka 30 kazini. **PICHA: PILLY KIGOME.**

Yupo Mariamu Shija (80), bibi anayetegemea ujira huo kugonga mawe ajilishe yeye na mume wake, asiyeweza kufanya chochote kutokana na umri mkubwa.

Anatamka kishatumikia kazi hiyo ya ugongaji kokoto kwa zaidi ya miaka 30, wakiwajibika bila kinga ya misimu yote; juani na kwenye mvua.

"Mjukuu wangu, mimi Mungu hajanijalia uzazi, sijazaa! Sina mtoto hata wa dawa wa kusema labda angenihurumia, nisifanye kazi hii ngumu nateseka sana.

"Lakini, nashukuru nanunua unga na mchicha nakula japo nguvu zimeshaniishia," anasimulia katika eneo la Kunduchi, Mtongani, Dar es Salaam.

Bibi Mariam, anasimulia alikuja jijini Dar es Salaam kutafuta maisha akitoka kwao mkoani Tabora, baada ya kuachika na mume wake wa kwanza, anayedai kisa ni baada ya kukosa uzazi wakiwa kwenye ndoa muda mrefu.

Hapo analalamika mateso, dharau na kebehi kutoka familia yake yakachukua nafasi, akisema ndiyo ikawa 'kisa na mkasa' kuachika.

Anataja ilikuwa zama za miaka ya 1970, ndipo akaamua kuingia katika tafsiri mpya ya maisha, kusaka mwelekeo ndani ya Dar es Salaam. Hata hivyo, hakumbuki mwaka mahsusi aliyoiacha Tabora, hadi kufika jijini.

Pia, akadokeza kaka yake aliyeenda Tabora akamshawishi wafunge wote safari kujaribu Maisha, Dar es Salaam, akaridhia.

**MAISHA MAPYA**

Anasimulia alifikia eneo la Tegeta kwa Masista kwa kaka yake, akaanza kujishughulisha na biashara ndogo kipindi hicho na kubahatika kuhifadhi fedha, akaweza kununua eneo la kipimo cha 'mti wa mkorosho' kwa shilingi 100, akajenga nyumba ya udongo, akaweza kuishi eneo hilo.

Miaka mingi baadaye, anasema akatokea mnunuzi kutaka eneo hilo, naye akapauza na hata kumuwezesha kujenga nyumba ya tofali na pakampatia makazi bora ya kudumu.

Anasema, miaka ya baadaye akaona ajiunge na shughuli ya ugongaji mawe kwa kushauriwa na mmoja wa jirani zake ili aweze kupata fedha ya kujikimu kimaisha.

Hata hivyo, anakiri amechoka sana kiafya, lakini hana mbadala wa kumpatia chakula kumsitiri, huku mume wake hajimudu kimaisha 'hata kiduchu'.

"Kwa sasa naweza kugonga ndoo nne tu napata shilingi 1000 kwa siku, narudi nyumbani," anasimulia.

**WAGONGAJI WENGINE**

Pia, mahali hapo pana mgonga mawe Batuli Masayanyika (60), mjane ambaye ni mkongwe katika shughuli hiyo, kwa miaka 20 sasa.

Amekutana na Nipashe hivi karibuni, naye akarudisha kumbukumbu zake mwaka 1994, alipoanza shughuli hizo eneo la Kunduchi Mtongani.

Mwasiti anasimulia kwamba wakati anaanza shughuli hiyo, alikuwa na mume ambaye kipato chake kilikuwa hakitoshelezi kuleta ustawi katika familia, ndipo alipoamua kujiunga na wanawake wengine kituoni hapo.

Mwasiti anasema, maisha yakasonga na miaka mingi baadaye, mume wake akafariki umri ukiwa umeshasonga na ili kuweza kujikimu kula na watoto, pia wajukuu na ndugu wa karibu wanaomtegemea, akajikita katika kazi hiyo

Inaendelea Uk 14

UCHUMI

# Akikaribia miaka minne; Samia na staili ya kusuka uchumi kwa nguzo za kiafya, siasa

## • Abuni vitendea kisekta vinavyomuwezesha kufikia dira

**Na Mwandishi Wetu**

ANAPOJUMUISHWA kiuchumi, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anabeba wasifu wa kuwa rafiki kuendesha taifa linalomea kibiashara, uwekezaji na uchumi imara katika taifa lilotulia.

Inapotajwa 'taifa lililotulia', ndani yake kuna dhana ya ustahimilivu kisiasa, kiafya na kijamii, ikiwamo katika nafasi ya pekee wa ajenda yake; ustawi wa kinamama, vijana na watoto.

Ndani ya ustawi wa msamiati kiswahili 'ukiona vinaelea, vimeundwa,' katika msimu wa sasa imebaki miezi michache ahesabu miaka minne ya urais wake, Dk. Samia mbali na kampeni za kisiasa na kiutawala, pia amekuwa akiunda misingi na nyenzo za utendaji serikalini, kufanikisha malengo hayo.

Hapo kuna sheria na itikadi, pia taasisi za kiutendaji zitazomsaidia kuunda Tanzania na Watanzania anaowataka.

Ni mwezi uliopita tu kukaribisha mwaka mpya 2025 na kuuaga 2024, usiku wa Desemba 31, akitoa salamu kwa Watanzania akafafanua undani wa kinachoendelea, pia mavuno yake:

Akataja uchumi wa nchi uliendelea kuimarika na kuwanufaisha Wananchi ambapo, kati ya Januari hadi Juni 2024, uchumi ulikua kwa asilimia, 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023.

"Deni la Taifa nalo liliendelea kuwa himilivu, mfumuko wa bei umebaki ndani ya lengo la asilimia tatu, hali iliyochangiwa na sera madhubuti za kifedha.

"Tulishuhudia ongezeko la uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi, kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania kati ya Januari hadi Novemba 2024.

"Tumesajili miradi ya uwekezaji 865 yenye thamani ya Dola za Kimarekani bilioni 7.7 inayotarajia kuzalisha ajira 205,000.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akikagua mwenendo wa ujasiriamali nchini, katika Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa nchini, mwaka jana, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO.**

"Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje (EPZA), imetoa vibali vya kuwekezwa nchini viwanda vipya vikubwa 15 vyenye thamani ya Dola za Marekani milioni 235, vinavyotarajia kuzalisha ajira karibu 6,000 na kuuza nje bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani milioni 94 kwa mwaka.

"Kwa upande wa mapato, Mamlaka ya ukusanyaji Mapato Tanzania (TRA) imefanikiwa kukusanya shilingi trilioni 21.276 kati ya mwezi Januari na Oktoba 2024, sawa na asilimia 99.3 ya lengo.

"Hili ni ongezeko la asilimia 17.5, ikilinganishwa na makusanyo katika kipindi kama hicho mwaka 2023," anasema.

**AONGOZA KIKAO TNBC**

Ni miezi mitano kabla ya hotuba hiyo, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaamua kuongoza Mkutano wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC), mnamo Julai 29.

Kimsingi, TNBC, ni jukwaa muhimu katika kujadili mazingira ya biashara, uwekezaji na uchumi kwa ujumla nchini.

Kupitia mkutano huo, akasisitiza agizo lake kuhakikisha mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) nchini inaboreshwa, inaunganishwa na kusomana ifikapo mwezi Disemba mwaka huu.

Hapo anaeleza ni kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi, kupitia mifumo ya kielektroniki na kuongeza kasi na uwazi katika utendaji kazi.

Ni msimamo aliyourejesha tena juzi akiwa Unguja katika shamrashamra za sherehe za Mapinduzi Zanzibar, alikosema katika shule moja, akitaja umuhimu wa Tehama na akasistiza ndio mwelekeo wa mtaala kwa wanafunzi wa sasa na mahitaji ya duniani iendako.

Akiwa katika mkusanyiko na wafanyabiashara mwezi Julai, akapokea maoni na mapendekezo yao,akiahidi serikali kuyafanyia kazi.

Naye akatoa wito kwa sekta binafsi, kuendeleza dhamira ya kufanya kazi na serikali kama mbia wao na sio mshindani, ili kwa pamoja waendelee kujenga taifa.

**PROGRAMU IMASA**

Katika nyenzo zake za kusuka taifa imara kiuchumi, akaunda nyenzo; Programu ya Imarisha Uchumi na mama Samia (IMASA) ikilenga kuwawezesha Wanawake, Vijana, Wazee na Makundi Mengine Maalum.

IMASA inatekelezwa katika mikoa 26 ya Tanzania Bara na mitano Zanzibar. Kwa upana, programu inatazama kuwawezesha wananchi kuzingatia rasilimali na malighafi zinazopatikana katika mkoa au eneo husika, mfano wafugaji kuwezeshwa kwenye eneo lao. Vilevile namna hiyo kwa wakulima na wachimbaji madini.

Programu ya IMASA inatekelezwa kuanzia katika ngazi ya vitongoji, mitaa, vijiji hadi ngazi ya Taifa.

Kazi kuu ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) ni kuratibu shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi nchini.

Hiyo inagusa kupitia mifuko na programu mbalimbali ya uwezeshaji, ushiriki wa watanzania katika uwekezaji, uendelezaji wajasiriamali, na kuratibu uwezeshaji katika mikoa na halmashauri mbalimbali nchini. Vilevile, baraza hilo linaratibu na kusimamia kuanzishwaji na uendelezwaji vituo vya uwezeshaji nchini.

Hadi sasa kuna vituo 25 vya uwezeshaji nchi nzima, kazi zake ni kusimamia, kuratibu na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu fursa za uwezeshaji nchini.

Baraza tajwa lina waratibu katika maeneo ya miradi yote mikubwa nchini, ikiwa na lengo la kusimamia ushirikishwaji na ushiriki wa wananchi katika shughuli za kimaendeleo.

Moja ya wajibu wa baraza ni kuandaa mikakati na miongozo mbalimbali ya uwezeshaji nchini kwa lengo la kuondoa urasimu na kurahisisha shughuli za kiuchumi nchini.

Baraza pia, linasimamia vikundi mbalimbali vya wajasiriamali nchini, pamoja na kuwaunganisha na fursa za kibiashara zinazopatikana ndani na nje ya nchi.

**NISHATI SAFI KUPIKIA**

Hadi sasa Rais Dk. Samia anasifiwa, kuwa mweledi wa kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, katika hicho kinachoitwa Azimio la Kizimkazi, Zanzibar.

Rais anatajwa kuonyesha hali ya kuwajali wanawake, kwa kuhakikisha wanapata nishati safi ya kupikia inayotunza mazingira yao.

Programu ya IMASA, matarajio yake itaibua vipaji katika makundi yote, kulingana na mazingara husika ikiwagusa; vijana, wanawake na wenye ulemavu, wachangamkie fursa ya IMASA.

Lengo la Rais Dk, Samia na serikali yake ni kuanzisha majukwaa hayo ya uwezeshaji, ili kuwainua wananchi kutoka uchumi wa chini kwenda ngazi ya kati, kuhakikisha taifa linakuwa na nguvukazi, yenye maendeleo.

**LISHE BORA & M-MAMA**

Vilevile mtazamo wa serikali hiyo, inagusa harakati za kuondoa udumavu wa afya, ikiwekeza katika lishe bora nchini, ikisambaza programu ya 'Lishe Bora kwa Watoto' katika ngazi ya vijiji hadi taifa.

Rais Dk. Samia, pia anadumu na kushikilia Programu ya Afya kwa Kinamama, inayoitwa 'M-MAMA' ambayo sasa mjamzito anapopata uchungu wa kujifungua, gari la wagonjwa linamfuata nyumbani, kumpeleka hospitali, ikipunguza adha ya mikasa mibaya inayoendana na kujifungua.

JICHO LA DIRA 2050...

# ULIPO MTAJI NA MWITIKIO WAO VIJANA, KUPATA MZIZI WA 'TANZANIA TUITAKAYO'

**Na Hamenyimana Ntalengwa, UDSM**

INAPOANGALIWA Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 iliyotolewa mnamo mwezi Desemba mwaka jana, inaangazia ifikapo safari yake, kuna malengo:

Inagusia Tanzania inayotarajiwa kuwa taifa lenye maendeleo yanayolingana na nchi zenye uchumi wa Kipato cha Kati, Ngazi za Juu na zaidi.

Rasimu hiyo inaweka wazi kuwa, ili kufikia hatua hiyo, kunahitajika mageuzi makubwa ikizingatiwa kuwapo ongezeko kubwa la watu wanaokadiriwa kufika milioni 140.

Kati yao, nusu ya idadi hiyo watakuwa wanaishi mijini na inatarajiwa wengi wao watakuwa ni vijana.

Mbali na makadirio hayo, hata leo ikirejewa Sensa ya Watu a Makazi ya Mwaka 2022, takwimu inaonesha idadi ya vijana kuwa kubwa, asilimia 34.5 ya Watanzania wote.

Moja ya eneo ambalo ni Mpango wa kuhakikisha kunafikiwa 'Tanzania Tuitakayo' kama ilivyotolewa Desemba 2024 kwenye dira hiyo ya maendeleo kusonga 2050, ni pamoja na kuwapo "ubora wa hali ya juu wa maisha na ustawi kwa wote."

Msingi wake ni kwamba, hakuna namna nyingine ya kuwa na ubora, bila ya kuwapo uvumbuzi na ubunifu. Kufikia ustawi huo, ni lazima ubunifu uweze kupewa nafasi kubwa ya kukuzwa katika kundi kubwa la watu linalotarajiwa kuongezeka kwa kasi wakati huo, likijumuisha vijana.

Ikirejewa nukuu za Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akatamka "ujana ni siha njema na bongo kali." Hapo alimaanisha kwamba, vijana hao wana uwezo mkubwa wa kufikiria.

Hivyo wana wajibu wa kutumikia fursa mbalimbali na kuonesha ubunifu walionao, pindi wanapopewa ushirikiano mkubwa na serikali, ili kuhakikisha "tunafikia Tanzania tuitakayo hata kabla ya 2050."

Ni jambo linawezekana kupitia uvumbuzi na ubunifu, ikiwa sehemu ya vichocheo muhimu vya maendeleo yao vijana, pia uchumi kwa maendeleo endelevu.

Kwa kuzingatia uwapo wa idadi kubwa ya vijana, suala la uvumbuzi na ubunifu linapaswa kupewa kipaumbele katika sera na mipango, kwa maslahi mapana ya vijana na maendeleo ya taifa.

Ni msingi unaozipa serikali na wadau, wajibu wao wa ulezi na usimamizi,

Inaendelea Uk 14

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Kamwe tusikubali mazingaombwe kwenye uchaguzi






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

ENZI hizo tukiwa shule za msingi, kila Alhamisi ya mwisho wa mwezi, mwalimu wa zamu alikuwa akitutangazia kuwa kesho Ijumaa, atakuja mtu kuonesha mazingaombwe, hivyo kila mmoja aje na kiingilio.

Nakumbuka alikuwa akija mchezesha mazingaombwe huyo aliyekuwa na asili ya bara Asia na kutuonesha mambo ya ajabu ajabu, ikiwa ni pamoja na kutafuna nyembe na kutapika sindano nyingi!

Tukiendelea kushangaashangaa, alikuwa akichukua karata na kuziunganisha kimaajabu na kuwa kama mkanda mrefu, nasi tukishangilia kuhalalisha kiingilio chetu.

Kana kwamba haitoshi, alikuwa akichanachana karatasi na kuzifikicha na ghafla kutoa leso nyingi na kuzigawa kwa baadhi yetu watazamaji, waliopata wakawa wamefidia viingilio vyao.

Siku moja katika maonesho hayo, tuliyoyaona kama ya kichawi, mwanamazingaombwe huyo, akaniteua mimi nishiriki onyesho la kupasua tumbo na kutoa chakula na kuniponya papo hapo.

Nashangaa sikuwa na woga, wala hofu, nilikubali na akanikalisha kwenye meza na kunilisha ndizi kibao na kuwaambia watazamaji kuwa punde atanipasua na kuzitoa ndizi nilizokula.

Watu walinyamaza katika chumba hicho cha darasa kwa hofu, wakiamini kuwa ulikuwa mwisho wa maisha yangu. Hakika nilibugizwa ndizi mpaka kitumbo ndi!

Baadaye akanilaza kwenye meza na kunifunika uso nisione kilichokuwa kikiendelea, huku akionya kuwa nikipiga kelele na hata watazamaji wakipiga kelele, basi safari ya mwisho ni kwa Muumba wangu.

Kwa hofu ya kiuanafunzi na hasa kitoto, nilitii amri na kulala nakuhakikisha hata sikohoi wala kupiga chafya, nikihofia maisha yangu kutoweka, huku wazazi nyumbani wakiwa hawajui nini kinaendelea.

Basi 'upasuaji' ulipoanza, nikahisi kama nafinywafinywa tumboni na mjanja aliyeteka akili zetu na mara akanibandika pamba nyingi tumboni, eti kuonesha kuwa kweli alinipasua na kutoa ndizi,

ambazo kweli nilipoamka nikaziona pembeni zikiwa zimesagwasagwa mithili ya zilizotafunwa na kumezwa.

Nilipoamka, wanafunzi wakashangilia kwa nguvu huku wengine wakinipongeza na kutaka kujua nilikuwa najisikiaje, lakini nami nikawa nawashangaa ingawa kwa hofu, lakini sikuthubutu kugusa tumbo nikihofia kufumua 'mshono'!

Na siku hiyo ndiyo lilikuwa onyesho la mwisho na kabla hajaondoka akanifuata na kunitaka nifuatane naye mpaka nyumba ya kulala wageni alikofikia, kwani hakuwa mkazi wa mji tulipokuwa tukiishi.

Walimu waliniruhusu, kwani muda wa kutawanyika ulishawadia, nikafuatana naye kwa kutembea kwa miguu mpaka alikokuwa amefikia, tukaingia chumbani mwake akanizolea sarafu nyingi alizokuwa nazo akanipa. Sikuamini!

Hata nilipofika nyumbani, nikamsimulia mama na kumwonesha zile pesa akashangaa na kunihoji nilikozipata, akafurahi sana, ingawa alinionya nisiwe najitia kimbelembele kufanyiwa majaribio kama hayo, kwani kuna siku wakikosea nami ndiyo basi.

Hata Jumatatu shuleni, wenzangu wakawa hawaamini kama ni mimi niliyepasuliwa.

Basi ndugu zanguni, mwaka huu ni mwaka mwingine wa mazingaombwe, mwaka wa watu kutafuta kura za kula. Ni mwaka ambao tutaoneshwa na kusimuliwa mengi mazuri ya kusadikika.

Watu wema wataongezeka ghafla, 'watoto' wataongezeka wa kutoa shikamoo za bwerere bila hata kujali umri, ili kubembeleza kono liende kinywani. Ni wakati wa mavuno kwa wapiga 'kula'.

Kama kawaida zile ahadi za mkinichagua nitaleta hiki na kufuta hiki na kile, na nitapambana na changamoto hizi na zile na mtaishi maisha mazuri ambayo hamjapata kuyaishi.

Zile kauli za tangu mwaka 1961 tulipopata uhuru mpaka leo zitatamalaki.Bila shaka mmeanza kusikia wenyeviti wa kamati za usalama za mikoa wameanza kupaza sauti dhidi ya wanaojipitisha majimboni kuomba kutambuliwa kama watia nia.

Marufuku zimeanza kupigwa huko, kwamba wabunge waliopo wasibughudhiwe, waachwe wamalize ngwe yao kwa usalama na watu wavute subira, ili muda ukifika wafanye yao.

Baadhi ya wabunge wanaolindwa na kauli hizo, ni ambao tangu wachaguliwe hawajatia mguu majimboni na kama wamekwenda ni bababisha bwege tu, ili kuuza sura.

Kuna wabunge na madiwani ambao wamediriki hata kuhama maeneo yao na kuishi kwingine, wakiwekeza miradi yao wakisubiri mwisho wa ngwe wavune kiinua mgongo watanue miradi.

Watia nia msirudi nyuma, mbele kwa mbele tu mpaka kieleweke, safari hii tunataka wabunge imara wanaojua shida za wananchi na si chawa wanaoshangilia na kusifu kila kitu, wakikodolea hisani za mamlaka ya uteuzi.

Wananchi tusikubali mazingaombwe tena, tusiwe tayari kulishwa ndizi na kupasuliwa feki, ili kudanganywa kuwa tunaletewa maendeleo, Tukipata wabunge wazuri ndipo tutapata serikali nzuri. Inshallah!

# Ulipo mtaji na mwitikio wao vijana, kupata mzizi wa 'Tanzania Tuitakayo'

Inatoka Uk 12

kuhakikisha kwamba vijana wanawezeshwa kwa kupatiwa ujuzi stahiki wa kuvumbua.

Pia, watakuwa wanabuni na kuibua kuibua vipaji hiyo, vishiriki kikamilifu katika elimu na uchumi unaoendeshwa na uvumbuzi na ubunifu ambao ndiyo msingi wa Mapinduzi ya Nne ya Viwanda.

**ENEO LA PILI**

Eneo la pili linalohitaji ubunifu mkubwa, hasa kutoka vijana walipo katika

malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, ikihitaji usimamizi thabiti na endelevu wa ikolojia.

Vijana hapo wanapaswa kuwa wabunifu katika kuhakikisha



Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alitamka "ujana ni siha njema na bongo kali". **PICHA: MTANDAO.**

ongezeko la uchafuzi wa mazingira na upotevu wa baadhi ya aina za viumbe hai kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi, yanapewa ufumbuzi na kutatuliwa.

Kundi hilo la vijana linanapaswa kuitikia kwa nguvu, ikibuni, kuvumbua na kuboresha njia za kuhakikisha ikolojia inabaki sawia, kuvipa viumbe vyote nafasi ya kuzaliana na kuongezeka.

Hapo inaendana na kupitisha vinasaba kwenye vizazi vijavyo, vikitunza ikolojia katika ngazi yake sawa, ndipo hata maisha ya binadamu na uzalishaji utazidi katika viwango vikubwa.

Kwani ndani ya ikolojiam ndiko kunapatiokana malighafi za kulisha viwanda vikubwa na vidogo, huku uchumi ukizidi kukua.

Jukumu la kufikia malengo yote ya Tanzania 'tuitakayo mpaka kufikia mwaka 2050' ni la watu wote, hata mwitikio wa vijana katika ubunifu ukiwa mkubwa bado watahitaji kupewa ushirikiano na serikali pamoja na jamii kwa ujumla.

Inajulikana, serikali ipo tayari kutoa ushirikianao mkubwa kwa vijana wanapokuwa na ubunifu wenye kuleta maendeleo ya taifa. Mfano hao unapatokana hata kuoptia majukumu ya taasisi ya kitaifa ya COSTECH, ambayo majukumu yake ya kila siku yamesimamia ngazi hiyo.

Pia umma, wakiwamo vijana, wana wajibu muhimu kuhakikisha wanadumisha amani na kuwapa nafasi ya kufanya ubunifu mbalimbali kama wana jamii, ilimradi wanayolibuni itufikishe kwenye "Tanzania Tuitakayo."

- ***Ni maoni binafsi ya kitaaluma ya mwandishi, ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa pili wa shahada ya kwanza, katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.***

# BIBI MIAKA 80, WAJANE, HADI VIJANA WAISHI KWA KUGONGA MAWE KOKOTO

Inatoka Uk 11

Anaielezea Nipashe kuwa, sasa anategemewa na watu zaidi ya wanne ambao wote wanamuangalia yeye kwa kipato hicho kisichozidi shilingi 3000 kwa siku.

Katika orodha hiyo, anawataja watoto wawili, pia wajukuu wawili, huku kukiwapo mtoto wa kaka yake alitokea mkoani Tanga na kuja nyumbani kwake, baada ya kushindwa maisha kijijini.

Anasimulia kipindi anaanza kazi hiyo mwaka 1994, walikuwa wanalipwa ujira wa shilingi 150 kwa ndoo, yenye vipande vya kokoto zitokanazo na jiwe lililogongwa.

Mwasiti anataja kiwango anacholipwa sasa kwa kila ndoo ni shilingi 250 na kwa siku huwa anamudu ndoo 10 ikimapatia shilingi 2,500.

Naye kama alivyonena mtangulizi wake Bibi Mariamu, Mwasiti analalamika ameshachoshwa na kazi hiyo, ila anashindwa kuacha kwa sababu ndio nguzo ya kipato chake na familia.

"Sina jinsi mwanangu, sina wa kunisaidia, kwani nikiacha hapa, wajukuu zangu watakufa njaa na wanaonitegemea hivyo nitafia kwenye hii kazi," anasema

Mwasiti anaeleza manufaa pekee anayoiona katika kazi hiyo ni ujira unaomlisha, tena akinena chakula cha gharama nafuu anachokitaja "kununua mboga za majani na unga hakuna faida nyingine!"

Anaendelea: "Mwanangu wa kiume kaachana na mkewe, watoto wake wawili kanileteа mimi. Nina mtoto wa kaka yangu wa kiume katokea Tanga... nae yupo siwezi kumfukuza kaka amefariki



Batuli Masayanyika (60), mjane mwenye miaka 20 ya kugonga mawe ya kokokoto akiwa kazini. **PICHA ZOTE: PILLY KIGOME.**

"Sisi tunakula, yeye anatuangalia haitawezekana na hata ukiweka ugali...mtoto wangu wa kike naye sio wa kumtegemea sana kwani na yeye hana mume na hana kazi."

Sasa anawaomba wamiliki wa mradi wanaotumukia, kuwaongezea ujira kutoka shilingi 250 za sasa, akisema awali alikuwa anagonga hadi ndoo 15 kwa siku. Lakini, akakwama kutokana na umri kumuacha.

Sharifa Bakari (55), anataja kuanza kazi hiyo mwaka 2014, akidumu na miaka 10 ya kupambania kula yake mahali hapo, kupitia ugongaji mawe ya kokoto.

Anaiambia Nipashe kuwa kazi hiyo ni ngumu, naye hana jinsi kutokana hali mapungufu ya kifedha na uhalisia wa udhaifu aliyo nayo.

"Mume ninaye, baba wa watoto wangu niliyezaa nae watoto watano, ila kwa sasa ni mtu mzima sana na mbaya zaidi hafanyi kazi yoyote ni mlemavu wa macho kwa hiyo hawezi kufanya kazi yoyote, ninalazimika kufanya kazi hii ili tule," anasema Sharifa.

Anasema, ana mnyororo wa watu watano wanaomtegemea akiwamo mume, pia mdogo wake wa kike, binti na mjukuuu mmoja, wote wanamtegemea yeye.

Nipashe ilipotaka kujua kulikoni hali hiyo kutegemwewa na kundi, akafafanua mbali na mume mlemavu, mdogo wake ni mlemavu asiyetembea na binti yake bado hajapata kibarua anachokitaja 'cha kueleweka.'

Anafafanua kuwa bintiye 'anahangaika Kariakoo' kusaidia Mamalishe kwa ujira duni, unaoishia kwenye usafiri, kutokana na umbali mrefu kutoka makazi yao.

Pia, ananena kuwa binti huyo kazalishwa na mwanaume aliyekataa mtoto huyo, akiitaja ni hali inayowaongezea uzito wa kimaisha.

Anasema mumewe awali alikuwa na shughuli zake za ulinzi, pia kiongozi wa kisiasa Kunduchi, lakini baadaye akapata ugonjwa na macho yakafa, huku umri umeshakuwa mkubwa.

"Sasa hapo ndipo nilipovurugwa zaidi, kwa kuwa awali tulikuwa tunasaidiana, lakini sasa hata yeye ananiangalia mimi, iwe jua iwe mvua, ni lazima nije nigonge kokoto, ili mradi tununue kilo ya unga na mchicha tule" anasema

Kamera ya Nipashe, katika dodoso hiyo, ihakahamia kwa Mariam Julius (36), anayejitambulisha yu mama wa watoto watatu, mumewe amefariki.

Anaitaja kuwa mazingira yaliyomfanya kujiunga na kazi hiyo kujikimu na wanawe, akisema "wanakula" pia, "wanaenda shule na matumizi madogo madogo ya kila siku anayapata kutokana na kazi hiyo."

Mgonga kokoto huyo mama kijana, anasimulia safari yake ya kijiunga na kundi hilo, ilianza baada ya kujikuta anasumbuliwa na maendeleo ya biashara yake, hasa kimasoko.

Anaeleza mitaji yake 'ilikatika' kila mara, huku wa kumasaidia amefariki, akaona aingie mbadala wa vibarua vya kuchekecha kokoto (kuzitofauatisha na udongo), akijaza ndoo moja analipwa ujira wa shilingi 200.

"Kutokana na kazi hiyo kwa siku nina uwezo wa kuchekecha ndoo 40 hadi 30 najipatia hela (Sh. 6,000 hadi Sh. 8,000) ya kwenda kula na wanangu," anasema Mariam.

Anataja changamoto kubwa anayokutana nayo kazini ni kipindi cha mvua kazi haifanyiki, kwa kuwa eneo hilo lote kunakuwapo tope na kokoto hata kukwamkisha uchekechaji mchanga kuwa mgumu.

**WADAU WAINGILIA**

Baada ya kubaini madhila wanayopata kinamama hao, taasisi isiyo ya kiserikali ya HIMA, iliiona kundi hilo la wanawake wagonga kokoto wa Kata ya Mtongani mkoani Dar es Salaam, wakawapa elimu ya ukatili wanawake hao wapatao 50.

Kaimu Mkurugenzi ambaye ni Ofisa Miradi, Hilda Msangi, anasema wakaona wawafikie wanawake hao kuwapatia elimu hiyo, waweze kujitambua wanapokuwa katika shughuli zao hizo

Hilda anasema, hiyo ni kutokana na ongezeko la vitendo vya ukatili majumbani, makazini na maeneo ya utafutaji riziki wa kila siku.

"Tumeona kundi hili kama limesahaulika, mashirika mengi hawawafikii, sisi tumeona tuwe mfano kulifikia kundi hili na mwandishi umeona ni jinsi gani wanawake hawa hawana uelewa mkubwa kuhusiana na ukatili," anafafanua Hilda.

Soviana Martin (30), mgonga kokoto katika eneo la Mbuyuni, anasema wanakabiliwa na changamoto nyingi, zikiwamo kukosa vifaa kazi kama vile

barakoa, mabuti, glovu, miamvuli ya kujikinga na jua na ukosefu wa vyoo Jirani yanayayowazunguka.

Nipashe ilipomfuata Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa Mtongani Stanslaus Thomas, kufafanua baadhi ya changamoto zinazomhusu, akakiri madai lao ya wagonga kokoto, ikiwamo kuwa katika kazi wakati mgumu kwa hitaji kama vyoo.

Akataja changamoto hiyo ni kubwa na yeye hana ufumbuzi wa moja kwa moja, kulingana na ngazi yake ya utendaji kikazi, ikizingatiwa shughuli hizo zinaendeshwa kando ya hifadhi ya barabara.





# Madaktari 120 wa mifugo wafutiwa usajili

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

BARAZA la Verterinari Tanzania (VCT) limewafutia usajili madaktari wa mifugo 120 nchini kwa kukosa sifa ya kutoa huduma ya afya ya mifugo.

Vilevile limetangaza kuwachukulia hatua madaktari watakaokaidi amri hiyo kwa kuendelea kutoa huduma hiyo kinyume na sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Msajili Msaidizi wa VTC, Dk.George Mtinda alitaja sababu ya kufuta usajili kwa madaktari hao kuwa ni kushindwa kulipa ada sh. 30,000 kwa mwaka kwa muda mrefu.

Mtinda, alisema baada ya baraza hilo kupitia majina ya wadaiwa, lilifikia uamuzi huo wa kuwafutia usajili. "Kikao cha baraza kililiidhinisha madaktari 120 kufutiwa usajili kwa kukosa sifa za utoaji huduma ya afya ya mifugo baada ya kulimbikiza madeni kwa muda mrefu," alisema.

**Kazi nyingine zitakazofanyika ni kufungua viwanda vya kuzalisha mvinyo wa asali, kujenga hoteli na viwanja vya mpira ili timu kubwa...**

Alisema kwa waliofutiwa usajili wanaweza kuomba tena kwa kulipa faini, ada na malimbikizo ya madeni waliyokuwa wanadaiwa kabla.

Mtinda alionya kuwa endapo watakaa nje kwa muda wa miaka miwili, watatakiwa kufanya mitihani ili wasajiliwe upya na kuendelea kutoa huduma.

Kwa mujibu wa Dk. Mtinda, ulipaji wa ada ni takwa la kisheria linataka madaktari hao kuhuisha usajili kila mwaka.

Katibu wa Chama Cha Madaktari wa Wanyama Tanzania, James Kawamala, alisema hatua ya kuwafutia usajili madaktari hayo ina athari kubwa katika jamii.

Alisema serikali imekuwa ikiwakumbusha mara kwa mara na chama kutekeleza jukumu lake lakini kumekuwa na uzembe.

"Kama chama tunaendelea kuhamasisha kulipa madeni ili kuepuka madhara ambayo yanaweza kujitokeza ikiwemo kufungiwa huduma na kupelekwa mahakamani.



Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Athumani Toto akizungumza na viongozi na wanachama wa majimbo yote ya mkoa huu jana, wakati wa kikao cha kupanga mkakati kuelekea mkutano mkuu wa uchaguzi wa chama utakaofanyika Januari 21, 2025.Katika mkutano huo walitoa tamko la mgombea uenyekiti wa Chadema taifa watakayemuunga mkono. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE.**

# Wafanyakazi TAKUKURU watakiwa kutunza siri

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Crispin Chalamila amewataka watumishi wa taasisi hiyo kutunza siri za ofisi na kufanya kazi kwa bidii ili kujenga imani kwa wananchi.

Chalamila, pamoja na kuipongeza taasisi hiyo kwa kufanya vizuri kuzuia rushwa, aliwasisitiza watumishi wake kuongeza jitihada zaidi ili kuwasaidia wananchi na kuleta maendeleo nchini.

Chalamila alisema hayo jana katika ziara ya kutembelea ofisi za TAKUKURU mkoani hapa na kuzungumza na watumishi kuhusu utendaji wa kila siku.

Alisema TAKUKURU ni taasisi muhimu mbele ya jamii, hivyo watumishi hao wanatakiwa kutekeleza majukumu kwa weledi.

"Nawapongeza sana kwenye eneo la uzuiaji rushwa, lakini nasisitiza jitihada ziongezeke,"alisema.

Aliwakumbusha kuhakikisha uchunguzi wanaofanya uendane na urejeshaji wa mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa nchini.

Alisema anaamini taasis hiyo iko vizuri kwenye uchunguzi na uendane na uhalisia majukumu yao ili kusaidia jamii kupiga vita rushwa.

"TAKUKURU tunaaminiwa na wananchi nasi tuonyeshe uaminifu wetu kwao kwenye utekelezaji wa majukumu yetu," alisema Chalamila.

Alisisitiza watumishi kukataa kushawishiwa na jamii kupokea rushwa wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Victor Swella, aliahidi wataendelea kufanya kazi kwa ushirikiano kudhibiti kuzuia rushwa.

Swella, alisema mikakati waliojiwekea ni kuhakikisha mapambano dhidi ya rushwa yataendelea kufanyika kwa kushirikiana na wananchi na kutoa elimu ya madhara ya vitendo hivyo katika jamii.

# REA wahamasisha nishati safi kupikia

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) unatarajia kusambaza mitungi ya gesi 19,530 ya kilo sita na vifaa vyake mkoani hapa kwa ajili ya kuhamasisha matumizi ya nishati safi kupikia na kuachana na nishati chafu.

Hayo yalisemwa jana na Kaimu Mkurugenzi Mkuu REA, Emmanuel Yesaya wakati wa uzinduzi wa mradi wa ugawaji wa mitungi hiyo kwa bei ya ruzuku iliyofanyika wilayani Chamwino.

Yesaya, alisema mradi huo unatarajia kusambaza mitungi hiyo kwa wilaya sita za mkoa huo kwa kila moja 3,255 kwenye maeneo ya pembezoni mwa miji na vijijini baada ya kusaini mkataba na Kampuni ya Lake Oil.Ω

Alisema REA wamebeba jukumu hiyo ikiwa ni kuunga mkono kampeni ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha utunzaji wa mazingira nchini kwa jamii kuacha kukata miti ovyo kwa ajili ya kupata kuni na mkaa kupikia.

"Lengo la mradi huu ni kukuza, kuchochea, kuwezesha na kuboresha upatikanaji wa huduma za nishati safi ya kupikia kwa wananchi na kuongeza maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini na pembezoni mwa miji," alisema Yesaya.

# Hisabati, Sayansi kufundishwa shuleni kwa mtandano

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MKOA wa Singida umeweka mkakati wa kutumia teknolojia ya kufundisha Sayansi na Hisabati kwa kuunganisha shule zote kwenye mtandao wa kompyuta ili walimu wachache wa masomo hayo waliopo waweze kufundisha shule nyingi. Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, alitangaza mkakati huo jana wakati akihojiwa na kituo kimoja cha redio cha mjini hapa kuhusu mambo mbalimbali yaliyoyofanywa na serikali kwa mwaka uliopita wa 2024 na mikakati kwa mwaka huu.

Dendego, alisema mkakati huo wa kutumia teknolojia hiyo kufundisha kwa masomo hayo, ifikapo Juni mwaka huu shule zote hususani za sekondari zitakuwa zimeunganishwa na kwenye mtandao wa kompyuta ili kukabiliana na upungufu walimu.

"Tumekuwa na upungufu wa walimu katika mkoa wetu hususani wa masomo ya sayansi, serikali kupitia vyuo vya ualimu imeendelea kuzalisha walimu na Singida tumekuwa tukipata mgao na tutahakikisha hakuna mtoto anayekosa somo fulani sababu ya upungufu wa walimu," alisema.

Dendego, alisema anatarajia kuitisha kikao cha walimu kuzungumza nao ili kukabiliana na tatizo hilo. Alisema pamoja na upungufu uliopo mkoani hapa, maeneo ya mijini kuna idadi kubwa ya walimu wakati vijijini wapo wachache . Alisema tatizo hilo litakwenda kupatiwa ufumbuzi katika kikao hicho ili kuweka uwiano sawa wa walimu katika shule zote kuanzia kata na vijijini.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato, alisema halmashauri zinajitahidi baada ya robo ya kwanza kukusanya asilimia 52 ambayo ni zaidi ya malengo ya kukusanya asilimia 50.

Aliziagiza halmashauri hizo kuendelea na ukusanyaji mapato hususani za Wilaya ya Iramba, Mkalama na Manispaa ya Singida.

Kwa upande wa wafanyabiashara, Dendego, aliwataka kutoa stakabadhi za malipo kwa wateja wanaponunua bidhaa katika maduka yao ili kushirikiana na serikali katika mnyororo wa kukusanya mapato.





# Mvua, kimbunga vyaacha maafa

**Na Elizabeth John,**
NJOMBE

NYUMBA 12 za mitaa ya Ikwete na Malombwe Kata ya Lyamkena Halmashauri ya mji Makambako zimeezuliwa paa na kusababisha wakazi wake kukosa makazi.

Nyumba hizo ziliezuliwa paa na mvua zilizonyesha zikiwa zimeambatana na upepo mkali Januari 3, mwaka huu na kusababisha wakazi wake kuomba hifadhi kwa ndugu na jamaa.

Mbali na watu hao kukosa makazi, mvua hizo zimeharibu vyakula na kusababisha mtoto mwenye umri wa miaka 15 kujeruhiwa kichwani.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mwenyekiti wa Mtaa wa Ikwete, Amon Neston, alisema nyumba tisa ziliezuliwa katika mtaa wake mvua hizo zikinyesha mchana.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Malombwe, Daniel Japhet, alisema katika mtaa wake nyumba tatu zimeezuliwa na kuiomba serikali na wadau kuwasaidia wakazi wake kwa kuwapa chakula na vifaa vya ujenzi.

**Kamati ya Maafa Halmashauri hiyo, imefika katika mitaa hiyo ya Ikwete na Malombwe kuwafariji waathirika wa maafa hayo.**

Baadhi ya waathirika wa maafa hayo akiwemo, Joyna Ndawala, aliiomba serikali na wadau kuwapatia msaada ili kukabiliana na hali ngumu kwa sasa.

Kamati ya Maafa Halmashauri hiyo, imefika katika mitaa hiyo ya Ikwete na Malombwe kuwafariji waathirika wa maafa hayo.

Mjumbe wa kamati hiyo ambaye pia ni Ofisa Mazingira, Gift Kivia alisema baada ya tathimini kufanyika watawasilisha kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya mji huo, Kenneth Haule ili waone namna ya kuwasaidia wananchi hao.

Jumla ya nyumba 32 na ofisi moja ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) zimeezuliwa paa na kimbuga katika Halmashauri hiyo toka msimu wa mvua wa 2024/2025 uanze.

Nyumba 13 ziliezuliwa Kata ya Mlowa Novemba 29 mwaka jana, saba na ofisi moja ya CCM Kata ya Utengule Desemba 14, mwaka huo na nyingine 11 katika Kata ya Lyamkena Januari 3, mwaka huu.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Dk Ashatu Kijaji akiwasili katika viwanja vya Majulai kata ya Mwangoi kwa ajili ya kuzungumza na Wananchi wa Jimbo la Mlalo, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto wakati wa ziara yake ya siku mbili katika Wilaya ya Lushoto. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Lushoto, Ally Daffa, akifuatiwa na Mkuu wa Wilaya hiyo Zephania Sumaye. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# TARURA yahadharisha wanaong'oa vibao vya mitaa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

WAKALA wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) mkoani Ruvuma imetoa tahadhari kwa wananchi wanaoharibu miundombinu ya barabara kwa kung'oa vibao vya majina ya mitaa.

Akizungumza na Nipashe juzi ofisini kwake, Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma, Silvester Chinengo, alisema kuwa wananchi wanatakiwa kutambua kuwa miundombinu ya barabara ni mali ya wote.

"Jukumu kubwa la wananchi ni kuhakikisha wanailinda miundombinu ili iweze kutumika kwa muda mrefu, vitendo vya uharibifu wa miundombinu ya barabara ni kinyume na malengo ya serikali," alisema .

Chinengo, alisema wananchi wanatakiwa kujua pia kutupa takataka kwenye maeneo ya mifereji na katikati ya barabara ni uharibifu wa miundombinu.

"Kuchimba mchanga kwenye maeneo ya madaraja, kingo za mito ni kuzorotesha hali ya usafi pamoja na uimara wa miundombinu hiyo," alisema .

Alifafanua kuwa TARURA inashirikiana na viongozi wa serikali za mitaa, vijiji, wilaya na mkoa kuhakikisha miundombinu ya barabara inatunzwa na kutumika kwa muda mrefu.

Chinengo, aliwahimiza wananchi kuwa walinzi wa miundombinu ya barabara iliyopo kwenye maeneo yao na kutumika kwa manufaa ya wananchi wote.

# Umeme wawaliza wakulima parachichi

**Na Mwandishi Wetu,**
NJOMBE

KUKOSEKANA umeme kwenye mashamba ya parachichi ya wakulima katika Halmashauri ya mji Njombe, kunadaiwa kukwamisha uzalishaji wa zao hilo kwa maji ya kuvutwa mabondeni kwa kutumia mashine.

Hayo yalisemwa juzi na baadhi ya wakulima wa zao hilo wakati wa ziara ya ya Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka ya kuangazia fursa za uzalishaji wa mbegu bora mkoani hapa.

Mmoja wa wakulima hao, Steven Mlimbila, alisema pamoja jitihada na mtaji mkubwa waliowekeza katika mashamba yao yaliyopo maeneo ya Kifanya, umeme ni kikwazo na kusababisha kukosa maji ya uhakika wakati wa kiangazi.

"Tunayo mashamba mengi, changamoto kubwa ni maji, tunaomba utusaidie umeme," alisema Mlimbila.

Alisema mbali na kuzalisha miche ya kisasa na ubora inayotegemewa na mataifa mengine, bado kuna Watanzania wanaagiza mbegu nje ya nchi na kukwamisha jitihada katika sekta ya kilimo Eligius Wella, aliliomba Shirika la Umeme nchini (TANESCO) kupeleka nishati hiyo katika maeneo ya uwekezaji wa kilimo hicho ili wawe na uhakika wa kuzalisha kwa tija.

Kwa upande wake, Mtaka, aliwataka Watanzania kutambua mkoa huo umewekeza kwenye ubora wa miche na mbegu za mazao mbalimbali, hivyo hakuna sababu ya kuhangaika kuagiza nje ya nchi.

"Ipo biashara ya miche Njombe na msipokuwa makini mtafanya biashara ya mzunguko kwa sababu mtu atanunua miche Tanzania ataipeleka Kenya, Uganda, Congo na Burundi halafu atajitangaza anazalisha. Kisha atanunua miche ya Njombe iliyopo Burundi na kuirudisha Tanzania kwenye shamba la Njombe," alisema.

Kuhusu kilio cha wakulima hao kukosekana kwa umeme, Mtaka alisema amekipokea na kuahidi kukifanyia kazi.

Ofisa Kilimo wa Mkoa huo, Wilson Joel, alisema Njombe inazalisha miche milioni 1.5 kwa msimu mmoja na kwamba hiyo ni fursa kubwa kwa wakulima na wananchi kuchangamkia kilimo hicho.

Ofisa Biashara wa Mkoa huo, Lusungu Mbede alisisitiza ubora katika uzalishaji wa miche na parachichi zenyewe kukubalika katika masoko yote duniani.





# Nyumba 3,000 za makazi kujengwa Chumbuni

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Nyumba Zanzibar linatarajia kujenga nyumba 3,000 za makazi katika mji wa Chumbuni visiwani hapa ili kuboresha maisha ya wananchi.

Mpango huo ulitangazwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Uchumi na Uwekezaji, Sharif Ali Sharif.

Sharif alisema shirika hilo, litajenga nyumba nyingine 24 katika eneo la Kiembe Samaki, 500 Kisakasaka, 120 Nyamanzi na maeneo mengine.

Alisema shirika hilo linajenga nyumba hizo za makaa, ikiwa ni mpango wa Serikali kuwaenzi waasisi wa Mapinduzi ya mwaka 1964 ya kuwapatia wananchi makazi bora na salama.

Sharif alitoa kauli hiyo wakati wa uzinduzi wa nyumba za makazi na biashara katika eneo la Darajani Mnadani mjini hapa.

Alisema jitihada hizo ziliendelezwa na viongozi kwa awamu tofauti kutoka ya kwanza hadi ya nane ili kutimiza lengo la Mapinduzi hayo ya Zanzibar.

**"Serikali imeweka vipaumbele vyake katika maeneo makuu manne ikiwemo huduma za jamii, miundombinu, utalii na uchumi wa buluu," alisema Sharif.**

Sharif, alisema Mapinduzi hayo yameleta mabadiliko makubwa kwa Zanzibar kwa sababu watu walikuwa wakiishi katika nyumba za udongo.

"Serikali imeweka vipaumbele vyake katika maeneo makuu manne ikiwemo huduma za jamii, miundombinu, utalii na uchumi wa buluu," alisema Sharif.

Alisema Shirika hizo limeanza kutekeleza ujenzi wa nyumba katika maeneo mbalimbali.

Alilipongeza shirika hilo kwa kutekeleza miradi ya nyumba hizo za makazi na kuboresha maisha ya wananchi.

Naibu Waziri wa Ardhi na Makazi, Salha Muhammed Mwinjuma, alisema Ilani ya Chama Cha Mapinduz (CCM) imeelekeza kujenga nyumba mpya 120 na kukarabati 300.

Mkurugenzi wa Shirika hilo, Sultani Said, alisema wamejikita kuwajengea wananchi nyumba za gharama nafuu kipindi kifupi kijacho.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera Bunge na Uratibu) William Lukuvi akiwa katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa jengo jipya la Mahakama ya wilaya ya Mkoani ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Miundombinu bandari Unguja, Pemba kuimarishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema Serikali inaendelea kuimarisha ujenzi wa miundombinu ya Bandari kwa Unguja na Pemba ili kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa.

Abdullah, aliyasema hayo katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Bandari ya Shumba Mjini ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya kutimiza Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema kukamilika kwa ujenzi wa bandari hiyo kutaimarisha huduma za usafiri wa baharini katika Mkoa wa Kaskazini Pemba kutokana na kuwa kiungo muhimu kati ya Bandari ya Tanga na Mombasa Kenya nchini Kenya .

Alisema ujenzi wa bandari hiyo na nyingine zinazojengwa Zanzibar utatoa fursa za ajira kwa wakazi wa visiwani hapa na kukuza uchumi.

Abdullah, alimuagiza mkandarasi anayejenga bandari hiyo kuongeza saa za kazi ili bandari kukamilika na wananchi kunufaika nayo.

Vilevile, aliwataka wananchi kuunga mkono juhudi za Rais Dk. Mwinyi za kuwaletea maendeleo na kudumisha amani na mshikamano nchini kwa kutokubali kuingizwa kwenye chuki za kisiasa kwa maslahi ya watu wachache wasioitakia mema Zanzibar.

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Khalid Salum Muhammed, alisema wizara yake inaendelea na ujenzi wa miradi ya barabara, viwanja vya ndege na bandari katika visiwa vya Unguja na Pemba ili kukuza uchumi wa nchi.

Dk. Khalid, alisema ujenzi wa miundombinu ya bandari una lengo la kuimarisha na kuboresha huduma ya usafiri na usafirishaji nchini.

Alisema Serikali inajipanga kupanua Bandari ya Mpigaduri kwa kujenga kituo cha usafiri wa teksi za baharini na kutua ndege za baharini.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa bandari hiyo, Katibu Mkuu Wizara hiyo, Dk. Habiba Hassan Omar, alisema hadi kukamilika utagharimu zaidi ya Sh. bilioni tano zilizotolewa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ).

# Waliojenga pembezoni mwa barabara kulipwa fidia

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amemuagiza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi kuwalipa fidia watu wanaomiliki nyumba kando ya barabara ili kunusuru maisha yao.

Dk. Mwinyi alitoa agizo hilo baada ya kuzindua barabara ya Micheweni Shumba bandarini na ya Kiuyu Maziwang'ombe Wilaya ya Micheweni, ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya mwaka 1964.

Alisema kumekuwa na tabia kwa baadhi ya wananchi wanapoona ujenzi wa barabara, wanajenga nyumba za makazi na kuleta changamoto kwa usalama wa maisha yao na kuwasihi kutoingia kwenye hifadhi ya barabara.

Mwinyi, alisema ahadi za ujenzi wa barabara za Micheweni Shumba ya mjini bandarini na Micheweni Kiuyu Maziwang'ombe imetimia baada ya kukamilika.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itaendelea kujenga barabara nyingine mpya za ndani kwa kiwango cha lami.

Alisema kuwa Wilaya ya Micheweni ahadi ambazo zilitolewa katika kipindi cha kampeni nyingi zimetimia baada ya baadhi ya barabara kujengwa.

Waziri wa Wizara hiyo, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema barabara hizo zinazojengwa ni za kisasa.

Mohamed, alisema baadhi ya watu ambao hawajazoea kushuhudia mambo ambayo yanafanywa na Serikali ya awamu ya nane wanaweweseka.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo , Dk. Habiba Hassan Omar, alisema

Barabara ya Micheweni Kiuyu Maziwang'ombe, Micheweni Shumba mjini bandarini ni miongoni mwa barabara zilizomo katika mradi wa ujenzi wa barabara za ndani unaoendelea Unguja na Pemba.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**TUNU BRAITONI SANGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S 4848-0083** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **AFRICAN RAINBON SECONDARY SCHOOL** mwaka 2013, Cheti cha chuo cha Ualimu Rukwa chenye index No. **E.05910174 , EA 160007645** Kilichotolewa na wizara ya Elimu mwaka 2016. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **RB PHQ/MBE/MBE/1356/2025**

## KUPOTEA KWA VYETI



**JANE MAKUBI MHANGILWA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S2565¬-0004** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MATABA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018, cheti cha diploma chenye namba **E0523-0048** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Monduli teachers college mwaka 2022, kitambulisho cha mpiga kura na Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0416-0610** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Monduli teachers college mwaka 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi **PHQ/MOR/MOR/1093/2025**

## KUPOTEA KWA VYETI



**NKWIMBA LAMECK MWANDU,** Mtajwa hapo juu amepotelewa na cheti cha Kidato cha NNE Shule ya Sekondari Mwakaluba chenye Property number **CS110035722** Kilichotolewa mwaka 2011 na BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA). Cheti cha kidato cha sita Shule ya Jikomboe Sekondari chenye Property number **AC140068265** kilichotolewa mwaka 2014 na BARAZA LA MITIHANI TANZANIA (NECTA). Cheti cha chuo kikuu pamoja na Full transcript, (CHUO KIKUU CHA JORDAN) chenye Property number 201710564. na Reg. number **2014/0566.** Taarifa ya upotevu wav yeti hivyo imetolewa kituo cha polisi na kupewa RB namba. **SIM/MEA/RB/54435/2023, SIM/MEA/RB/54444/2023, SIM/MEA/RB/54453/2023**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**EMMANUEL PETER CHEREHANI**

naomba kutangaza kupotelewa na hati yangu ya kusafiria namba **TDE013347** iliyotolewa uhamiaji makao makuu Mwaka 2022 . Yoyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/SHI/KAH/406/2025.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MASOUD YUSUPH** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S 2502-0166** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MBWENI SECONDARY SCHOOL** mwaka 2011, Cheti cha kidato cha sita chenye index No. **S 0438-0514** Kilchotolewa na baraza la mitihani la Taifa kupitia **MASJID QUBAH MUSLIM SEMINARY** mwaka 2014. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi:**PHQ/DAR/KIN/7374/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JACKLINE NG'OCHA MAHONA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha Sita chenye Index No. **S0380/0503** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **UCHAMA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2018,. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/TEM/7357/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MWITA ELIAS MUSA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye Index No. **S2721/0071** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KEMAKORERE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MAR/TAR/342/2025**

## KADI ZA GARI ZIMEPOTEA

Ndugu **RAJABU YUSUPH MDEMU** anatangaza kupotelewa kwa kadi za gari zenye usajili ufuatao; **T.846 CDT na T.979 EFB .** Kwa yeyote atakayeziona anaombwa kutoa taarifa kwenye kituo chochote cha Polisi kilicho karibu.
Taarifa Polisi:
**PHQ/DAR/UBU/287931/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 02/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU ATHUMANI I. KIDILLEH wa NDUKA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AISHA A. KIDILLEH**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 20 Mwezi 01 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 02 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na.5/2025**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MNYAROPE BAYA CHILIGO wa MAJENGO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA SAID ATHUMANI KIJIKO**

**TANGAZO**
**(Kanuniya 5(2) ya Kanuniza Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 21 Mwezi 01 Mwaka 2025 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo Tarehe 08 Mwezi 01 Mwaka 2025

HAKIMU

## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

**RAPITECH SOLUTIONS LIMITED** kwa idhini tuliyopewa na **LOLC Tanzania Financial Services Ltd,** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kwa mdaiwa Khalid Saidi Mkanya wa Dar Es Salaam kulipa deni lake. Baada ya hapo hatua nyingine za kisheria zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na uuzwaji wa mali ulizoweka dhamana ya mkopo uliochukuliwa kama ilivyotangazwa gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| Khalid Saidi Mkanya | Toyota CANTER, Reg. No. T.616 EEL - Yard ya dalali (Kinyerezi) | 24/01/2025 | RAPITECH SOLUTIONS LTD |

**Masharti Mengine:-**
1. Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena.
2. Gharama za kuona, kukagua na gharama zingine zote za kuhamisha umiliki na kumtoa mdaiwa/mpangaji ni juu ya mnunuzi.
3. Kwa yeyote atakayeharibu au kuvuruga mnada hatua zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yake

**Mawasiliano piga:**
**RAPITECH :0628866132/ 0755264606**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Risasi zarindima Ikulu, hofu yatanda kuhusu rais

**N'DJAMENA, Chad**

HALI ya wasiwasi imetata kuhusu usalama wa Rais wa Chad, Mahamat Idriss Deby, baada ya risasi kurindima katika Ikulu ya nchi hiyo Jumatano ya wiki hii.

Hata hivyo, Waziri wa Mambo ya Nje wa nchi hiyo alijitokeza haraka na kuelezea wanajeshi wanaomlinda rais wamethibitisha kiongozi huyo yuko salama na taifa hilo liko chini ya udhibiti. Katika urushianaji wa risasi watu 19 wamethibitika wameuawa.

Taarifa hiyo ya wizara ilitangaza kuwa vikosi vya usalama vilifanikiwa kuzima jaribio hilo ambalo limetafsiriwa kama lilitaka kuvuruga nchi.

Tukio hilo lilitokea baada ya milio ya risasi kuripotiwa karibu na ofisi ya rais katika mji mkuu, N'Djamena.

Hata hivyo, jeshi liliimarisha ulinzi kwa kufunga barabara za karibu na eneo hilo.

Msemaji wa serikali Abderaman Koulamallah, alionekana kwenye video iliyorekodiwa katika makao makuu ya rais, akisema kuwa hali iko shwari, ingawa hakutoa maelezo ya kina kuhusu kilichotokea.

„Ilikuwa tukio dogo, kila kitu kiko shwari"Jaribio hili lote la kuvuruga nchi limezimwa."alisema kwenye video iliyochapishwa kwenye Facebook.

Kwa mujibu wa chanzo cha usalama, tukio hilo lilielezewa kama jaribio la shambulio la kigaidi.

„Watu waliokuwa kwenye magari matatu walishambulia kambi za kijeshi karibu na ofisi ya rais, lakini jeshi liliwadhibiti," kilisema chanzo hicho kwa masharti ya kutotajwa jina.

Koulamallah, akiwa na bastola kiunoni na akizungukwa na wanajeshi waliobeba bunduki za mashambulizi, aliahidi kutoa maelezo zaidi baadaye.

Milio ya risasi ilisikika kwa dakika kadhaa karibu na makazi ya rais, ikizua hofu kuhusu usalama katika eneo ambalo lina historia ya mapinduzi ya kijeshi.

Mkazi mmoja, Zakaria Daoud, aliye karibu na eneo hilo, alithibitisha kusikia milio mikali ya risasi.

Mkazi mwingine, Abbas Mahamout Seid, ambaye alikuwa karibu na eneo hilo akiwa kwenye pikipiki, alieleza tukio hilo: „Nimekwama Place de Nation mbele ya ofisi ya rais kwa sababu nasikia milio mikali ya risasi na kuona magari ya kijeshi yakija kutoka pande zote."

Jaribio hilo la shambulio lilitokea wakati kunafanyika ziara rasmi ya Waziri wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi.

Ziara hiyo ilifuatia uamuzi wa Chad kusitisha makubaliano ya ushirikiano wa ulinzi na mshirika wake wa muda mrefu, Ufaransa.

Ufaransa hapo awali ilitoa mchango muhimu katika kuisaidia Chad kupambana na wapiganaji wa Kiislamu katika eneo la Sahel lenye migogoro magharibi na kati mwa Afrika.

Rais wa sasa wa Chad, Mahamat Deby alichukua madaraka mwaka 2021 baada ya kifo cha baba yake, Idriss Deby, ambaye aliitawala nchi hiyo kwa zaidi ya miongo mitatu kufuatia mapinduzi ya kijeshi mwanzoni mwa miaka ya 1990.

Licha ya kuwa na utajiri wa mafuta, Chad inasalia kuwa moja ya nchi maskini zaidi barani Afrika.

Shambulio hilo lilitokea takriban wiki moja baada ya Chad kufanya uchaguzi wa bunge uliolenga kurejesha demokrasia. Hata hivyo, vyama vya upinzani vilikataa kushiriki uchaguzi huo, na matokeo bado hayajatangazwa.

***DW***



Wahamiaji waliojaa kwenye boti ndogo wakifurahia kuzaliwa mtoto wa kiume siku ya Jumatatu ya wiki hii. **PICHA: REUTERS**

## Ajifungua ndani ya boti iliyojaa wahamiaji haramu

**CANARY, Hispania**

MWANAMKE kutoka Afrika, amejifungua mtoto wa kiume kwenye boti lililojaa wahamiaji, wakati wakisafiri kuvuka bahari ya Mediteranian kuelekea kisiwa cha Canary nchini Hispania.

Taarifa iliyotolewa na timu ya uokoaji, ilisema boti hiyo ilionekana kwa mara ya kwanza Januari 6, ikielea baharini karibu na kisiwa cha Lanzarote.

Walinzi wa pwani waliifuatilia boti hiyo iliyojaa wahamiaji wanaokimbilia Ulaya kusaka maisha bora, na baada ya kuifika walikuta mtoto kazaliwa dakika chache zilizopita.

Siku mtoto huyo alizaliwa, Uhispania ilikuwa ikisherehekea Sikukuu ya Epifania.

Nahodha wa boti ya uokoaji, Domingo Trujillo, alisema walipata taarifa kuwa ndani ya boti hiyo kulikuwa na mwanamke mjamzito, lakini walipofika walishtuka walipokutana na mtoto aliyezaliwa dakika chache zilizopita.

Mama na mtoto walikimbizwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa huduma za ziada za matibabu katika kisiwa cha Lanzarote.

Hata hivyo, wote walikuwa na afya njema, kwa mujibu wa mamlaka ya kisiwa hicho.

Kamanda wa kikosi cha uokoaji wa helikopta alielezea kuwa kuzaliwa kwa mtoto ilikuwa zawadi bora zaidi waliyopokea siku hiyo.

Safari ya kuvuka bahari kutoka Afrika hadi Visiwa vya Canary ni hatari kutokana na kupoteza maisha ya watu wengi baharini, mwaka jana pekee zaidi ya wahamiaji 46,800 walifanya safari hiyo.

***BBC***

**Nahodha wa boti ya uokoaji, Domingo Trujillo, alisema walipata taarifa kuwa ndani ya boti hiyo kulikuwa na mwanamke mjamzito, lakini walipofika walishtuka walipokutana na mtoto aliyezaliwa dakika chache zilizopita.**

# Ujerumani, Ufaransa zamuonya vikali Trump

**BERLIN, Ujerumani**

Ujerumani na Ufaransa zimemuonya rais mteule wa Marekani, Donald Trump, kuhusu nia yake ya kukinyakua kisiwa cha Greenland, eneo ambalo liko chini ya Denmark.

Kansela wa Ujerumani, Olaf Scholz alisema katika taarifa yake kuwa kanuni ya kuheshimu mipaka inatumika kwa kila nchi, haijalishi ikiwa ni ndogo sana au yenye nguvu sana.

Kwa upande wa Waziri wa Mambo ya Nje wa Ufaransa, Jean-Noël Barrot, alisema hakuna shaka kwamba Umoja wa Ulaya hautaruhusu mataifa mengine kushambulia mipaka yake.

Jumane ya wiki hii, Trump alisisitiza nia yake ya kukichukua kisiwa cha Greenland, akisema kisiwa hicho kilichopo Arctic ni muhimu kwa usalama wa kitaifa na kiuchumi.

Alielezea mara kwa mara kuwa anataka kukinunua kisiwa hicho baada ya kuliweka wazi wazo hilo 2019, wakati wa muhula wake wa kwanza kama rais.

Denmark ambaye ni mshirika wa muda mrefu wa Marekani, ilisema kwamba kisiwa cha Greenland hakiuzwi na ni mali ya wakazi wake.

Waziri mkuu wa Greenland, Mute Egede, ambaye anataka kisiwa hicho kiwe huru kutoka kwa Denmark, alisema eneo hilo haliuzwi

***BBC***

# KMKM hesabu kali mzunguko wa pili

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Mkuu wa KMKM SC, Ame Msimu, amesema malengo yake kwa sasa wakati huu wa mapumziko ni kupata mechi nyingi za kirafiki ili kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya kujiandaa na mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu Zanzibar.

Ligi hiyo kwa sasa imesimama ili kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea Kisiwani Pemba.

KMKM SC ipo katika nafasi ya saba ikiwa na pointi 23 baada ya kucheza michezo 14, imeshinda michezo sita, sare michezo mitano na wamefungwa michezo minne.

Akizungumza na gazeti hili jana, Msimu, alisema wakati uongozi wa timu hiyo unaendelea na mazunguzo juu ya usajili mdogo wa wachezaji, timu hiyo inaendelea kujifua kwa sababu wanataka kurejea na nguvu mpya katika mzunguko wa pili.

Msimu alisema hawakuwa na mwanzo mzuri katika mzunguko wa kwanza hivyo wanahitaji kurekebisha makosa kuelekea hatua ya lala salama.

"Ili kukifanya kikosi changu kiwe tayari na hatua ya pili, ninatarajia kupata michezo ya kirafiki ambayo tukicheza ninaamini itatupa mwanga kuelekea mzunguko wa pili wa ligi ambao utaamua hatima ya kila timu," Msimu alisema.

Aliongeza katika usajili huo mdogo amependekeza kuimarishwa zaidi katika eneo la ulinzi pamoja na safu ya ushambuliaji ili kuifanya timu kujilinda na kufunga mabao ambayo yatasaidia kutuma matokeo mazuri.

"Hatukua na mwanzo mzuri msimu huu, sasa ni lazima tufanye usajili mzuri kwa kuangalia mapungufu ya mzunguko wa kwanza, tunaangalia tulikwama wapi, tunahitaji kupata wachezaji ambao wataziba mianya kulingana na mapitio ya michezo iliyopita," aliongeza kocha huyo.

Aidha alisema timu hiyo tayari imeshaanza mazoezi yake kwa wachezaji ambao hawashiriki michuano ya Kombe la Mapinduzi.

"Kwa sasa wachezaji wangu wana ari kubwa hali inanimpa matumaini huenda mambo yakawa mazuri pale Ligi Kuu itakaporejeaendelea, kila mmoja anataka kuipambania timu ili kumaliza msimu kwenye nafasi za juu," kocha huyo alisema.

KMKM haiko katika mbio za kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar msimu huu kutokana na matokeo mabaya waliyopata katika mzunguko wao wa kwanza ingawa lolote linaweza kutoka kwenye mzunguko wa pili.

# MABAO 264 YAFUNGWA LIGI KUU MZUNGUKO WA KWANZA

**Na Adam Fungamwango**

JUMLA ya mabao 264 yamefungwa katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imemaliza mzunguko wa kwanza hivi karibuni huku baadhi ya timu zikiwa zimeshacheza michezo ya hatua ya lala salama ya ligi hiyo.

Kwa mujibu wa dawati la takwimu za michezo Nipashe, idadi hiyo ya mabao imefungwa katika michezo 127 iliyochezwa mpaka sasa.

Takwimu zinaonyesha katika michezo hiyo, mechi 94 zimetoa washindi na 33 zimeishia kwa timu kugawana pointi.

Katika michezo 94 ambayo timu zimeshinda, mechi 58 timu zimepata ushindi zikicheza kwenye viwanja vya nyumbani na mechi 36 zimetoa washindi wakicheza kwenye ardhi ya ugenini.

Wakati Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa imesimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi, fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa wachezaji wa ndani (CHAN) na mechi za kimataifa za hatua ya makundi ya michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

Mshambuliaji wa Singida Black Stars, Elvis Rupia, bado anaongoza kwa orodha ya upachikaji mabao akiwa amefunga magoli nane, akifuatiwa na Jean Ahoua wa Simba mwenye mabao saba, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate FC na Clement Mzize wa Yanga, kila mmoja amefunga mabao sita.

Wachezaji Leonel Ateba wa Simba, Edgar William (Fountain Gate), Pacome Zouzoua na Prince Dube (Yanga), pamoja na Peter Lwasa wa Kagera Sugar, wote wamefunga mabao matano kila mmoja.

Kwa upande wa utoaji pasi za mwisho, Feisal Salum wa Azam FC, anaongoza akiwa mpaka sasa, akifuatiwa na Ahoua wa Simba na Salum Kihimbwa wa Fountain Gate, wote wakiwa wametoa pasi za mwisho tano, huku wenye 'asisti' nne kila mmoja ni Stephane Aziz Ki, Mzize na Zouzoua, wote wa Yanga, pamoja na Josephat Arthur wa Singida Black Stars.

Wachezaji waliofunga mabao mengi ya penalti mpaka sasa ni Mcameroon Ateba, Ahoua wote wa Simba na Fei Toto' ambao kila mmoja amefunga matatu.

Aziz Ki wa Yanga amepachika penalti mbili wavuni mpaka sasa, Mourice Chukwu wa Singida Black Stars na Erasto Nyoni wa Namungo, kila mmoja ana mabao mawili ya mikwaju hiyo.

Hadi Ligi Kuu Tanzania Bara inasimama, Simba yenye pointi 40 ndio vinara wakifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 39.



Kiungo na nahodha wa Timu ya Kituo cha TFF (TDS),Mary Siame (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa Boni Consilli Girls kutoka Uganda katika mechi ya mashindano ya Wasichana ya CAF U-17 (GIFT) iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi. TDS ilipata ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: TFF**

# Fountain Gate yatema watatu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Fountain Gate imetangaza kuachana na wachezaji wake watatu lakini pia ikijipanga kusajili nyota wengine wapya ili kukiimarisha kikosi chao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Pia Mkenya, Robert Matano, anatajwa kurithi mikoba wa aliyekuwa Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohamed Muya.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo jana imesema wachezaji walioachwa ni Yesaya Hebron, Vitalis Nkosi na Aron Lulambo.

"Tunashukuru sana, tunasema asanteni kwa mchango wenu mkubwa ndani ya timu yetu. Tunawatakia mafanikio makubwa katika hatua zao zinazofuata na daima watabaki kuwa sehemu ya familia yetu," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Hata hivyo, Fountain Gate ndiyo timu iliyoruhusu mabao mengi katika mzunguko wa kwanza, nyavu zake zimetikiswa mara 32, kitu ambacho kimeonekana kuwakera mabosi wa timu hiyo na kuahidi kukiboresha kikosi.

Tayari timu hiyo imeshamtimua Muya dakika chake baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya mabingwa watetezi, Yanga uliochezwa, Desemba 29, mwaka jana kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam kwa kuchapwa mabao 5-0.

"Kuna mchakato unaendelea ndani ya timu, itakapokuwa tayari huenda akatangazwa kocha, Robert Matano, raia wa Kenya kuongoza timu yetu," kilisema chanzo chetu.

Matano amewahi kufundisha AFC Leopards, US Nakuru, Sofapaka FC na Tusker zote za Kenya.

HABARIMICHEZO

## ZISIKUPITE

### DIALLO KUZEEKEA UNITED
MANCHESTER United wamefikia makubaliano ya kumpa mkataba mpya, Amad Diallo, raia wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 22. ***(ESPN)***

### MAINOO, GERNACHO SAFI
KIUNGO wa kati wa England, Kobbie Mainoo, mwenye umri wa miaka 19 na winga wa Argentina, Alejandro Garnacho (20), wote bado wana nafasi ya kuendelea kubakia Manchester United, licha ya wasiwasi wa kukiuka sheria za faida na uendelevu (PSR). ***(Sky Sports)***

### MBEUMO SOKONI ENGLAND
MSHAMBULIAJI wa Brentford na Timu ya Taifa ya Cameroon, Bryan Mbeumo, mwenye umri wa miaka 25, yupo katika orodha ya wachezaji wanaowania uhamisho wa majira ya joto. ***(Florian Plettenberg)***

### MC ATEE AGOMBEWA ULAYA
KLABU za Ujerumani, Bayer Leverkusen, RB Leipzig, Mainz, Borussia Dortmund na Stuttgart zote zinamwinda kiungo wa kati wa Manchester City na England, James McAtee, mwenye umri wa miaka 22. ***(Telegraph)***

### CITY YAMTAKA MARMOUSH
MANCHESTER City bado inamtaka, Omar Marmoush, mwenye umri wa miaka 25, ambaye thamani yake ni pauni milioni 50, lakini huenda wakapata shida kumpata mshambuliaji huyo wa Misri kutoka Eintracht Frankfurt Januari hii, huku klabu hiyo ya Ujerumani ikipigania nafasi ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Guardian)***

### AINA AKARIBIA CITY
MANCHESTER City pia wanafikiria kumnunua beki wa Nottingham Forest na Timu ya Taifa ya Nigeria, Ola Aina, mwenye umri wa miaka 28. ***(GiveMeSport)***

### RONALDO KUMVUTA CASEMIRO
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, anataka kuungana na mchezaji mwenzake wa zamani wa Manchester United, Casemiro mwenye umri wa miaka 32, na ameiomba klabu ya Al-Nassr kumnunua kiungo huyo wa Brazil. ***(Mirror)***

### KHUSANOV KUTUA CITY
KLABU ya Manchester City imepiga hatua katika mazungumzo ya kumsajili beki wa Uzbekistan, Abdukodir Khusanov, mwenye umri wa miaka 20. ***(Team Talk)***

### ANTONY : SIENDI OLYMPIAKOS
WINGA wa Brazil, Antony mwenye umri wa miaka 24, amekataa nafasi ya kujiunga na klabu ya Ugiriki ya Olympiakos, lakini bado anataka kuondoka Manchester United. ***(Mirror)***

### HALL ATAJWA WEST HAM
WEST Ham inavutiwa na kiungo wa England, Kiernan Dewsbury-Hall, mwenye umri wa miaka 26, na huenda wakashinikiza mkataba wa mkopo na Chelsea. ***(Independent)***

### ZINCHENKO ANUKIA MILAN
INTER Milan inaandaa ofa ya kumnunua mlinzi wa Timu ya Taifa ya Ukraine na Arsenal, Oleksandr Zinchenko, mwenye umri wa miaka 28. ***(Sun)***

### JERMAINE KUTUA VILLA
KLABU ya Aston Villa inamfuatilia winga wa Borussia Dortmund, Jamie Jermaine Bynoe-Gittens, mwenye umri wa miaka 20. ***(Caught Offside)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WAARABU WANAJIPANGA SALAH AMRITHI NEYMAR

Mchakato huo unatarajia kuanza mapema kwa sababu mabosi wake...

**RIYADH, Saudi Arabia**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu ya Saudia Arabia, Al Hilal wamechagua kumsajili, Mohamed Salah kama mbadala bora wa Neymar, ambaye anatajwa kuelekea kuunganishwa tena na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona kule Inter Miami, kwa mujibu wa ripoti.

Uhamisho wa gharama kubwa wa Neymar kwenda Saudi Arabia haujazaa matunda.

Baada ya kuondoka Paris Saint-Germain kwa ada ya karibu dola milioni 90 mwaka 2023, raia huyo wa Brazil amekuwa fiti kwa mechi saba tu za mashindano.

Mkataba wa Neymar unamalizika msimu wa joto - ingawa kuna chaguo la kuongezwa kwa mwaka mmoja - na Al Hilal wanafikiriwa kumwachia aondoke.

Na sasa wanamwona, Salah wa Liverpool kama ndio jina bora kuchukua nafasi ya Neymar, kwa mujibu wa gazeti la AS la Hispania.

Sawa na Neymar, Salah anatazamiwa kuwa mchezaji huru ifikapo Julai na tayari anaweza kuanza kufanya mazungumzo ya uhamisho wa bure.

Salah mwenye umri wa miaka 32 anafurahia kiwango bora zaidi cha maisha yake ya soka Ligi Kuu England, lakini amesisitiza mara kwa mara huu ni „mwaka wangu wa mwisho" ndani ya Liverpool kutokana na hali ya sasa ya mazungumzo ya mkataba kusuasua.

Wakati klabu kadhaa za Ulaya, kama vile PSG na Barcelona, zimekuwa zikionyesha nia ya kumtaka Salah, Ligi Kuu ya Saudia imebaki na nia ya muda mrefu ya kumnasa nyota huyo wa Misri.

Hafez Al Medlej, mkuu wa zamani wa kampuni ya masoko na fedha ya ligi hiyo na mtu maarufu ndani ya Shirikisho la Soka la Asia, alisema hapo awali: „Lazima tuanze kufanyia kazi usajili wa Mohamed Salah kwa sababu ni maarufu sana katika ulimwengu wa Kiarabu na Ulaya."

Wakati Salah akionekana hana mustakabali kule Liverpool bado haijulikani, Neymar amekuwa akihusishwa sana na kuhamia klabu Ligi Kuu ya Marekani katika Klabu ya Inter Miami, ambapo anaweza kuunganishwa tena na wachezaji wenzake wa zamani wa Barcelona.

Lionel Messi, Luis Suarez na Neymar waliunda moja ya safu bora ya ushambuliaji yenye nguvu katika historia ya soka la kisasa.

Watatu hao kwa pamoja walifunga jumla ya mabao 122 wakiwa Barcelona na kushinda mataji matatu, LaLiga, Copa del Rey na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2014/15.

Katika mahojiano na CNN wiki hii, Neymar alikiri: „Ni wazi, kucheza tena na Messi na Suarez litakuwa jambo zuri zaidi. Ni marafiki zangu, bado tunazungumza mara kwa mara. Litakuwa jambo la kuvutia kucheza nao tena. Nina furaha na Al Hilal, nina furaha nikiwa Saudi Arabia, lakini ni nani anayejua kesho yake."

# Diallo apewa mkataba mpya United

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imekubali kumpa mkataba mpya, Amad Diallo, kwa mujibu wa ESPN.

Winga huyo mwenye umri wa miaka 22 ametia saini nyongeza ya muda mrefu ili kubakia hapo Old Trafford, taarifa rasmi la klabu hiyo ilitolewa jana.

Amad amepata umaarufu mkubwa Old Trafford msimu huu na kuwa mchezaji muhimu wa kocha mpya, Ruben Amorim.

Amad amefunga mabao sita katika mechi 28, likiwamo bao la kusawazisha katika sare ya mabao 2-2 dhidi ya Liverpool, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Anfield Jumapili iliyopita.

Mkataba wake ulitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, ingawa United walikuwa na chaguo la kuongeza mkataba wake kwa miezi 12.

Klabu iliamua kutoanzisha chaguo hilo na badala yake ikachagua kujadili mkataba mpya wa muda mrefu.

Amad alivumilia mwanzo mgumu wa uchezaji wake katika kikosi hicho cha United.

Aliwasili kwa mkataba wa pauni milioni 37 kutoka Atalanta mwaka 2020 na baadaye akapelekwa kwa mkopo Rangers na Sunderland.

Alifanya vyema katika klabu hiyo, akifunga mabao 14 katika michezo 42 wakati wa kampeni za msimu wa 2022-23.

Alishinda tuzo ya mchezaji bora chipukizi wa mwaka wa Sunderland na tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa mashabiki.

Amad amefunga mabao matatu katika mechi sita zilizopita akiwa na United, ukijumuisha bao la ushindi dakika za mwisho dhidi ya Manchester City Desemba, mwaka jana.

# Olmo, Víctor ruksa kuitumikia Barca

**BARCELONA, Hispania**

DANI Olmo na Pau Víctor wamepewa usajili wa kucheza kwa muda huku mahakama kuu ya michezo ya Hispania ikiendelea kuchambua kesi ya Barcelona dhidi ya LaLiga na Shirikisho la Soka la Hispania, (RFEF).

Mahakama kuu ya michezo ya Hispania (CSD) imeamua Olmo na Víctor wote wasajiliwe kwa muda hadi kuwe na uamuzi mahususi katika kesi hiyo.

Wote wawili hawakuwapo katika kikosi cha Barcelona kilichoshinda 2-0 dhidi ya Athletic Club kwenye Kombe la Super Cup Jumatano.

Lakini katika taarifa ya LaLiga ilisema haikubaliani na uamuzi wa CSD na kusema inafikiria kukata rufaa.

"Yaliyomo katika azimio hilo yatachunguzwa kwa makini ili kuwasilisha rufaa zinazofaa," ilisema taarifa hiyo.

Baada ya ushindi wa Super Cup, Kocha, Hansi Flick, alisema ilikuwa ahueni kubwa kwa upande wake kabla ya mchezo huo.

"Nina furaha sana kwa hawa watu wawili, lakini pia nina furaha kwa timu nzima," alisema Flick.

"Baada ya taarifa, unaweza kuona kinachotokea ndani ya basi, ilikuwa nzuri. Nadhani klabu nzima ina furaha sana kwa uamuzi huu.

"Olmo na Victor wana furaha. Sio mimi tu nina furaha, pia wana furaha. Ilikuwa ni ishara nzuri kwetu kabla ya mechi kwa sababu kila mmoja anataka kuonyesha pia sisi ni timu na tunashinda pia kwa ajili yao."

Olmo na Víctor wote hawakusajiliwa na LaLiga Desemba 31, mwaka jana baada ya Barça kutoweza kuthibitisha hawakukiuka sheria za ligi ya usawa wa kifedha (FFP).

Hatimaye LaLiga ilithibitisha Barca walikuwa wameonyesha walitimiza mahitaji fulani ya FFP Januari 3, mwaka huu na, kwa hiyo, "wameongezea muda wao wa matumizi."

Hata hivyo, katika taarifa yake ya pamoja na RFEF, LaLiga iliongeza wachezaji waliofutiwa usajili hawawezi kusajiliwa tena na klabu kwa mara ya pili katika msimu huo huo.



# MWAMUZI AMKASIRISHA VAN DIJK LIVER IKILALA

**LIVERPOOL, England**

MLINZI wa Liverpool, Virgil van Dijk, alikasirishwa na uamuzi wa mwamuzi wa kutompa kadi ya pili ya njano nyota wa Tottenham Hotspurs, Lucas Bergvall, kabla ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 kufunga bao pekee katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Carabao wakati ya timu hizo zilipokutana, juzi usiku.

Stuart Attwell, mwamuzi aliyechezesha mchezo huo awali alimwonyesha kadi ya njano, Bergvall kwa kumchezea vibaya, Luis Díaz, na akamwacha raia huyo wa Sweden alipomkwatua, Kostas Tsimikas aliyekuwa akitengeza shambulizi.

Mashambuliaji ya Liverpool yalipoisha, Attwell hakumwonyesha kadi ya pili njano Bergvall na muda mfupi baadaye kijana huyo alifunga, Alisson baada ya kazi nzuri kutoka kwa Dominic Solanke huku Tsimikas akiwa nje ya uwanja akipatiwa matibabu.

"Ilikuwa dhahiri kungekuwa na kadi ya pili ya njano," alisema Van Dijk akiiambia Sky Sports baada ya mchezo.

"Ilikuwa wazi, halafu dakika moja baadaye anafunga bao la ushindi. Sikiliza, ndivyo ilivyo. Mwamuzi alifanya makosa kwa maoni yangu na nilimwambia hivyo. Anadhani hakufanya hivyo. Ilikuwa wazi kabisa na kila mtu aliona.

"Hata VAR haikuonyesha chochote. Sisemi hii kwa sababu sisi kupoteza, lakini ilikuwa wakati muhimu katika mchezo."

Kocha wa Liverpool, Arne Slot, aliunga mkono maoni ya Van Dijk, akisema: "Uamuzi aliofanya mwamuzi huyo ulikuwa na athari kubwa kwenye matokeo usiku huo."

Mechi ya mkondo wa pili itachezwa Februari 6, mwaka huu kwenye Uwanja wa Anfield.

HABARI MICHEZO

# PAMBA JIJI YAOTA MAKUBWA, NYOTA WAPYA WAFIKIA SABA

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kuhakikisha inajiimarisha na kuwa na kikosi imara kwa ajili ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Pamba Jiji imefanikiwa kumsajili kiungo mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Burundi, Shassir Nahimana, imefahamika.

Taarifa iliyotolewa na Pamba FC jana imesema Nahimana amesajiliwa na timu hiyo akitokea Bandari inayoshiriki Ligi Kuu ya Kenya na inaamini atakuwa na msaada katika timu yao.

Ilisema pia klabu inaendelea kuimarisha kikosi chake kwa kuongeza nguvu katika maeneo yote yaliyokuwa na mapungufu.

"Tunatangaza rasmi tumemsajili kiungo mshambuliaji wa timu ya taifa ya Burundi na nahodha wa Bandari ya Kenya, Shassir (Nahimana). Amejiunga nasi katika kipindi hiki cha dirisha dogo la usajili akitokea Bandari, ambapo alikuwa tegemezi, akihudumu kwa miaka mitano kwenye kikosi cha Burundi," ilisema sehemu ya taarifa ya klabu hiyo.

Nahimana anakuwa mchezaji wa saba kutua Pamba kipindi cha dirisha dogo linalotarajiwa kufungwa ifikapo Jumatano ujayo.

Wachezaji wengine ambao wamesajiliwa na Pamba Jiji mpaka sasa ni kiungo mshambuliaji, Zabona Mayombya kutoka Prisons, beki wa kushoto, Cherif Ibrahim (Coton Sport ya Cameroon), winga, Deus Kaseke (huru), mastraika, Hamad Majimengi na Habib Kyombo kutoka Singida Black Stars, lakini pia ikiwa imempata kwa mkopo kipa, Mohamed Kamara, kutoka Singida Black Stars.

Mpaka kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Pamba Jiji inashika nafasi ya 14 ikiwa na pointi 12 kibindoni, imecheza michezo 16 na kati ya hiyo imeshinda miwili, imepata sare michezo sita na kupoteza minane.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo imesimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, mechi za michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, pamoja na Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itarejea tena ifikapo Machi Mosi.

Hadi ligi hiyo inasimama, Simba yenye pointi 40 ndio vinara ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Yanga yenye pointi 39, kila timu ikicheza michezo 15.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi ya Fountain Gate Tawi la Dar es Salaam wakicheza muziki katika sherehe za ufunguzi wa Mashindano ya Wasichana ya CAF U-17 (GIFT 2025), yanayofanyika kwenye Uwanja wa Azam Complex, jijini. **PICHA: CAF**

# JKT Queens: Tutalinda heshima

**Na Shufaa Lyimo**

MSHAMBULIAJI wa JKT Queens, Winfrida Gerald, amesema atapambana kuhakikisha timu yake inapata ushindi katika kila mechi watakayocheza katika mashindano ya Wasichana ya CAF U-17 ( GIFT), yanayoendelea kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Winfrida alifunga mabao mawili katika ushindi wa magoli 3-0 kwenye mechi ya ufunguzi dhidi ya KAS kutoka Kenya iliyochezwa juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Winfrida, alisema licha ya mashindano hayo kuwa na upinzani, lakini wamejiandaa kufuata vyema maelekezo wanayopewa na kocha wao ili kutimiza malengo.

"Malengo yangu ni kushinda michezo yote ili tuibuke mabingwa wa mashindano haya, tunaomba mashabiki waendelee kutuunga mkono, bila wao hatuwezi kufanya lolote," alisema mshambuliaji huyo.

Alisema wanashukuru kwa kuanza vyema michuano hiyo na wamejipanga kuendelea kusaka ushindi ili kusonga mbele katika michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza.

"Tulipata ushindi kutokana na kufuata vizuri maelekezo tuliyopewa nje na ndani ya uwanja kabla ya kuanza kwa mashindano, tutaendelea kupambana katika kila mechi, hatutadharau timu yoyote," alisema Winfrida.

Aliongeza anafurahishwa na ushindani unaonyeshwa na wasichana katika mashindano hayo jambo ambalo linampa matumaini ya kuona soka la wanawake linazidi Afrika Mashariki na Kati linakua.

## Simba SC, Yanga zagongana 'airport'

INATOKA UK. 24

kufanya. Al Hilal ni timu nzuri na hatari, lakini tumefanya kazi ya kuiangalia na kuangalia ni jinsi gani tutakwenda kucheza nao katika mechi hii," alisema Moalin.

Mechi nyingine ya Kundi A itawakutanisha MC Alger ya Algeria ambayo inashika nafasi ya pili ikiwa na pointi tano TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo), ambayo inaburuza mkia ikiwa na pointi mbili.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, amesema wanakwenda kucheza mchezo wa ‚kimkakati' dhidi ya wenyeji Bravo do Maquis ya Angola kwa sababu hautakuwa rahisi kutokana na nafasi ya wapinzani wao.

Fadlu alisema wanakwenda kucheza mechi hiyo kwa uangalifu mkubwa kwa sababu wanahitaji kumaliza dakika 90 wakiwa wamefuzu hatua ya robo fainali.

„Itakuwa ni mechi ngumu na ya tofauti sana, tunakwenda kucheza na timu ambayo ni nzuri sana ikiwa nyumbani kwao, huwa wanamiliki sana mchezo.

Tunatakiwa kuwa makini, tunatakiwa tuwe waangalifu, tukiwa na mpira na kipindi ambacho hatuna, kwa maana hiyo tunakwenda kucheza kimkakati, nia ni moja tu tusipoteze mchezo, tushinde au tupate sare," alisema kocha huyo.

Akiichambua Bravo do Maquis, alisema ni timu ambayo ikiwa kwao imekuwa na rekodi ya kushinda mabao mengi, lakini yenyewe pia ikiruhusu nyavu zao kutukiswa, hivyo wanatakiwa kuutumia vyema udhaifu huo ili kudhibiti nguvu zao.

"Ukiangalia ni timu ambayo inafunguka ikiwa kwao, ndiyo maana inafunga mabao mengi na kuachia mianya ya wao kuruhusu, lakini sisi hatuingii katika mtego huo, hatuwezi kufunguka kama wao wanavyocheza na kupishana nao, kwa sababu hicho ndicho kilichosababisha CS Constantine ya Algeria na CS Sfaxien ya Tunisia kufungwa mabao matatu kila moja, sisi itabidi tuwe waangalifu sana, tutapishana nao, tutawadhibiti na kutumia udhaifu wao kuwaadhibu," alisema kocha huyo.

Naye Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema ingawa wanahitaji pointi moja ili kusonga mbele, lakini wao hawaendi kusaka sare, badala yake wanataka ushindi katika mchezo huo wa Jumapili.

"Tunakwenda kupambana kwa ajili ya kuingia robo fainali, lakini ukweli hatuendi kufanya kazi nyepesi kwa sababu mpinzani wetu naye ana nafasi, akishinda na yeye anajiweka kwenye nafasi nzuri, na mpinzani wetu anaonekana amewekeza sana kushinda nyumbani, kifupi Jumapili ni kama mechi ya fainali ya Kundi A kwenye Kombe la Shirikisho.

Mahesabu yanaonyesha sisi tunahitaji pointi tatu au moja, na katika mpira wa miguu ni ngumu sana kuisaka pointi moja, sisi tunakwenda kusaka tatu na ikishindikana ndiyo tupate moja," Ahmed alisema.

Simba ipo katika nafasi ya pili kwenye msimamo wa kundi lao ikiwa imezidiwa na wastani wa mabao ya kufunga na kufungwa dhidi ya vinara, CS Constantine mwenye pointi kama hizo, ambayo nayo siku hiyo hiyo, itakuwa nyumbani kucheza dhidi ya CS Sfaxien.

# Michezo

Ijumaa Januari 10, 2025

Nipashe


Waarabu wanajipanga Salah amrithi Neymar

UKURASA 21



# Simba SC, Yanga zagongana 'airport'

## ●●●Tambo zatawala huku kila mmoja akikiri wana kibarua kizito...

**Na Adam Fungamwango**

SIMBA na Yanga zote za jijini, Dar es Salaam zimekutana kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere jana alfajiri, kila mmoja akiwa anaelekea katika majukumu ya mechi ya mashindano ya kimataifa ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF), zitakazochezwa keshokutwa katika viwanja viwili tofauti.

Simba inayoshiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho imeelekea mjini Luanda, Angola kuwafuata wenyeji Bravos do Maquis wakati Yanga wao wanaenda kupambana na Al Hilal ya Sudan ambayo inacheza michezo yake ya kimataifa kwenye Uwanja wa De la Capitale jijini Nouakchott, nchini Mauritania.

Akizungumza na gazeti hili muda mfupi kabla ya kuanza safari, Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe, alisema kwa sasa wanahitaji zaidi miguu ya wachezaji ifanye kazi kuliko maneno.

Kamwe alisema yanaweza kuzungumzwa maneno mengi, lakini ukweli kwa sasa walipofikia hawahitaji maneno zaidi ya wachezaji wao kuonesha vitendo kwa kupambana uwanjani kwa ajili ya kutafuta ushindi.

„Wachezaji wanatambua nini wanatakiwa kukifanya, nimepata bahati ya kuzungumza nao wamesema wanajua jukumu walilonalo na namna gani wanachama na mashabiki wanawategemea.

Mimi naweza kuzungumza maneno mengi, lakini ukweli tunahitaji miguu ya wachezaji zaidi na si maneno. Tunahitaji mguu wa Prince Dube, Stephane Aziz Ki, Ibrahim Hamad ‚Bacca' na Dickson Job ifanye kazi tupate matokeo mazuri,“ alisema Kamwe.

Aliongeza katika mchezo huo wanahitaji ushindi tu kwa sababu hata matokeo ya sare hayawezi kuwasaidia, hivyo ni ushindi ndiyo utawarudisha katika matumaini ya kutinga hatua ya robo fainali kutoka Kundi A.

“Hautakuwa mchezo mwepesi na sisi hatutauchukulia kiwepesi, tunafahamu tunacheza na timu ngumu, kinara kwenye kundi letu. Tuna pointi nne tunakwenda kupambana na Al Hilal, tukishinda tutakuwa tumeweka karibu zaidi matumaini yetu ya kutinga hatua ya robo fainali, si mechi ya fainali, ila itatusogeza mbele, tunajua jamaa pamoja na kwamba wamefuzu, lakini watataka kushinda ili wawe kwa kwanza.

Unapokuwa wa kwanza kwenye kundi unakuwa na faida mbili, kwanza unakutana na timu iliyomaliza nafasi ya pili kutoka kundi lingine, ya pili utaanzia ugenini na kumalizia nyumbani, hii ni faida kubwa sana katika michuano hii ya kimataifa, kwa hiyo mechi yetu pia wataitolea macho,“ Kamwe aliongeza.



Chama



Debora

Mkurugenzi wa Ufundi wa Yanga, Abdihalim Moallin, alisema uzoefu wa wachezaji wa Yanga, unawapa matumaini ya kushinda mchezo huo wa ugenini.

“Tunakwenda kusaka pointi tatu, natumaini tutazipata, wachezaji wetu hawana presha kwa sababu wameshacheza mechi nyingi kubwa, msimu uliopita walicheza michezo kama hii, wanajua jinsi gani ya

INAENDELEA UK. 23

# Wydad macho yote kwa Mzize, Aziz Ki

**Na Somoe Ng'itu**

KLABU ya Wydad Athletic ya nchini Morocco imeendelea kuwasilisha maombi ya kutaka kumnunua mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize, lakini sasa imeongeza ikisema pia inahitaji huduma ya Stephanie Aziz Ki, imeelezwa.

Katika taarifa iliyotolewa na Wydad inasema wako tayari kulipa ada ya Dola za Marekani 800,000 kwa kila mchezaji ili ajiunge na timu yao inayoshiriki Ligi Kuu ya Morocco.

Hata hivyo mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga imewajibu Waarabu hao kuwa wachezaji hao hawauzwi kwa sababu ya ushiriki wa timu yao kwenye mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika wanayoshiriki.

“Hatuko tayari kuwauza wachezaji hawa kwa sababu ya ushiriki wetu katika mashindano ya CAF ya Ligi ya Mabingwa na tuna nafasi ya kutinga hatua ya robo fainali,“ ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Kocha Mkuu wa Wydad, Rulani Mokwena, ameieleza Bodi ya Wakurugenzi wa timu hiyo kuwa anawahitaji wachezaji hao ili kuongeza nguvu katika kikosi chake.

Mokwena alianza kuvutiwa na wachezaji hao tangu akiwa na Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, ilipokutana na Yanga katika michuano hiyo ya CAF.

Yanga, wawakilishi pekee wa Tanzania waliobakia kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika itashuka dimbani huko Mauritania keshokutwa kuwakabili wenyeji Al Hilal na endapo itashinda mechi hiyo itajiimarisha kwenye mbio ya kusaka tiketi ya kutinga hatua ya robo fainali.

Al Hilal yenye pointi 10 na vinara wa Kundi A wameshafuzu hatua ya robo fainali na Yanga yenye pointi nne inahitaji ushindi tu ili kuendelea na kampeni yao katika michuano hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >